ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nne - Tarehe 28 Novemba, 2016

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Zuberi Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani ya Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya 2005, Kuweka Masharti Bora zaidi, kwa ajili ya Ufanisi na Usimamizi Imara wa Mfuko na Mambo Yanayohusiana na hayo.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani kuhusu Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya 2005, Kuweka Masharti Bora zaidi, kwa ajili ya Ufanisi na Usimamizi Imara wa Mfuko na Mambo Yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 137

Ujenzi wa Ofisi za Jimbo kwa Wawakilishi

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamepatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Jimbo na kwa kuwa baadhi yao wamejenga na wengine hawakujenga kabisa ofisi hizo mpaka leo.

Je, Serikali ni lini itawapa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi fedha za ujenzi wa ofisi za Jimbo kwa yale majimbo ambayo hayana ofisi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 137 kama ifuatayo:-

Mhe. Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano imekuwa na utaratibu wa kujenga Ofisi katika kila Jimbo kwa ajili ya matumizi ya Wabunge wa Majimbo hayo. Baadhi ya Majimbo ambayo Ofisi hizo zimeshajengwa ni Majimbo yaliyopo Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na kutambua umuhimu wa kuwepo kwa Ofisi hizo kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, bado Serikali ya Mapinduzi ya Zanziabr haijaanza ujenzi wa Ofisi hizo. Hii inatokana na gharama kubwa zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hizo kwa Majimbo yote ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, aidha, serikali hivi sasa imeweka mkazo zaidi katika kuleta maendeleo kwenye majimbo kwa kugharamia Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo kwa kila jimbo, kwa majimbo yote ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, hata hivyo, pale hali ya kifedha itakapoimarika, serikali italifanyia kazi suala la ujenzi wa Ofisi za Jimbo kwa Majimbo yote ya Unguja na Pemba. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote wana haki sawa, na kwa kuwa katika majibu mama alikiri kwamba ujenzi wa ofisi hizi utachukua pesa nyingi.

Je, serikali haioni kwamba watowe fedha hizi kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa awamu, kama walivyofanya kwa wengine.Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, serikali imeona ipo haja ya kuwa na ofisi hii, ndio maana hata katika jibu langu la msingi nilisema, pale ambapo hali ya fedha itaimarika basi tutakuwa na uwezo sasa wa kujenga ofisi hizo. Ingawa kwa sasa serikali imeona kuliko kuweka *impute* zaidi katika kujenga ofisi, ni vyema kasma ile kwa kila jimbo tuzielekeze katika suala zima la Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, hasa kwa dhamira ya kutaka kuwasaidia wananchi wetu

katika kila jimbo, badala ya kuwa na majengo pasi na kutoa huduma kwa wananchi, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, baadhi ya ofisi za wabunge kule Pemba hazitumiki ipasavyo, yaani vitendea kazi.

Je, una mpango gani kama serikali kuhakikisha kwamba zinatumika kwa kupitia sisi Wawakilishi tuliokuweko kule Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, serikali kwa kupitia Bunge ilikuwa na dhamira kwanza kuanza kujenga ofisi hii, kujenga ni hatua moja, lakini matumizi ni hatua nyengine. Sasa suala la matumizi ya ofisi hizi, kwanza inatokana na wabunge wenyewe ambao wanatoka katika majimbo yao, pale wanapoona ipo haja ya kutumia ofisi hii, serikali ilikuwa na nia hiyo, ndio maana kuna baadhi ya majimbo huko Bara hawakubahatika kuwa na ofisi hizi kwa sababu ya kile ambacho Mhe. Mwakilishi atakuwa amekiona. Sasa kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kweli hawatumii ofisi hizi kama vile inavyotakiwa, lakini dhamira njema ya serikali ilikuwa ofisi hizi zitumike kutatua matatizo ya wananchi kuliko kwenda kwa njia nyengine zaidi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza niipongeze Serikali ya Muungano kwa kuhakikisha kwamba wabunge wetu wanapata ofisi zao na kufanyia kazi, ambapo tunaamini kwamba kwa Zanzibar tunaweza kushirikiana na Wawakilishi bila ya matatizo.

Pili, niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuandaa mpango mzuri ambapo hapo baadae Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tutaanza kupata Mfuko wa Maendeleo kwa ajili ya kuendesha majimbo yetu. Swali langu liko hapa.

Je, kwa kuzingatia ofisi hizo ambazo baadhi ya majimbo hatuna kabisa. Kwa mfano Jimbo langu la Kijitoupele na majimbo mengine ya jirani, kama Fuoni, Pangawe na kwengineko. Mfano, je, wizara kwa kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ina mpango gani wa kuhamasisha kwamba na Wabunge wa

majimbo haya wapate uwezo wa kupata fedha hizo kujenga ofisi zao, ili tuwe karibu zaidi na wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kweli nakubaliana naye, kuwa yapo baadhi ya majimbo hapa kwetu Zanzibar Unguja na Pemba, hayana ofisi hizi za wabunge, lakini ipo sababu.

Mhe. Spika, mwaka 2015 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuja na kasi mpya ya majimbo, kasi ya majimbo ile ilifanya baadhi ya majimbo kutokuwepo nje ya ofisi hizo za wabunge. Sasa niseme tu kwamba wabunge wanakila sababu ya kwenda kulisema hili katika Bunge tukufu, ili Bunge sasa lione haja kwa kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuja kujenga ofisi hizo katika baadhi ya majimbo ambayo Mhe. Mwakilishi, ameyataja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 134

Kutofanya Kazi Kwa Chombo cha Taifa cha Majadiliano

Mhe. Said Omar Said - Aliuliza:-

Katika mwezi wa Machi 2016, Serikali kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma iliunda chombo cha kitaifa cha majaadiliano katika Sekta ya Umma. Chombo hicho kimeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 80 cha Sheria No. 2 (2011) na Kanuni za Utumishi wa Umma 2014.

Je, ni sababu gani zinazopelekea chombo hicho kutokufanya kazi tangu kuzinduliwa kwake Machi 2016.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 134 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Chombo cha Majadiliano cha Taifa ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011, chini

ya kifungu cha 80, kwa lengo la kuishauri serikali katika kutatua migogoro ya waajiri na waajiriwa kila inapojitokeza.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 70 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, chombo hicho kimepewa majukumu ya kuishauri serikali katika mambo yafuatayo:-

a) Mazingira mazuri ya kazi;

b) Mahusiano mazuri baina ya waajiri na waajiriwa;

c) Kutoa mapendekezo kwa serikali kuhusu tija na ufanisi na utowaji wa huduma bora kwa watumishi wa umma;

d) Kufuatilia rufaa itakayotolewa kutokana na shauri lililofikiwa na vyombo vingine vya kisheria vya majadiliano juu ya maslahi ya watumishi na;

e) Kukubaliana kuhusu suala jengine lolote ambalo washiriki wa makubaliano wataona inafaa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, chombo cha majadiliano kilizinduliwa tarehe 18/3/2016 na hadi sasa kimefanya kikao kimoja tarehe 21/11/2016. Kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizoanzisha, chombo hicho hakikuwekewa muda na utaratibu maalum wa uendeshaji wa vikao vyake.

Mhe. Spika, kwa kuwa ofisi yetu inaendelea na utaratibu wa kuzipitia Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 kuwa kuweka miongozo, hatua ambayo inatarajiwa kuweka utaratibu mzuri wa uendeshaji wa vikao vya chombo hicho.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafsi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kutokana na umuhimu wa chombo hiki, na kwa kuwa hata fungu sijaliona kwenye bajeti.

Je, serikali itakiwezesha chombo hiki lini ili kuweza kufanyakazi zake ipasavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa kuwa chombo hiki ni miongoni mwa vyombo vya serikali, suala la bajeti bila shaka litazingatiwa na wakati wowote kuanzia sasa inawezekana ikaingizwa kwenye bajeti ijayo.

Nam. 148

Wilaya za Unguja Kutumia Majina ya Asili

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa majina ya Mikoa na Wilaya za Unguja hazitumii majina ya asili ya maeneo husika kama zilivyo Wilaya za Pemba (Mkoani, Chake Chake, Wete na Micheweni).

Je, lini serikali itabadilisha majina ya Mikoa yote kwa Wilaya za Unguja, kuwa katika majina yake ya asili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 148, naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, suala la majina na mipaka inayoigawa Zanzibar ni la dahari nyingi na lina historia ndefu inayoonyesha kuwa kabla ya kuja kwa watawala wa kigeni, watawala wenyeji wa enzi hizo kama akina Mwana wa Mwana kwa maeneo ya Tumbatu, Mwinyi Mkuu kwa maeneo ya Unguja Ukuu, Bi Khole kwa maeneo ya Bungi, Mkamandume kwa maeneo ya Pujini Pemba na wengineo walikuwa na maeneo yao ya kiutawala.

Mhe. Spika, kuja kwa utawala za kigeni utaratibu ulianza kubadili mifumo na maeneo ya kiutawala ambapo mnamo mwaka 1926 Sheria ya *Native Decree of* 1926 ilianzisha utawala katika ngazi ya Shehia. Tabaan, Shehia za wakati huo ni tafauti na hizi za sasa kwa idadi, mipaka na hata majina. Sheria nyengine ya *District Administrative Authority Decree of* 1926 iligawa Zanzibar katika Mikoa mitatu (wakati huo ikiitwa Wilayat) ambayo ni Mkoa wa Mjini, Mkoa wa Mashamba na Mkoa wa Pemba. Aidha, Wilaya kumi nazo zikaanzishwa (wakati huo zikiitwa Mudiriyat).

Mhe. Spika, baadhi ya Wilaya hizi zilibeba majina ya maeneo halisi na mengine bado yanaendelea kutumika hadi sasa. Upande wa Unguja kulikuwa na Wilayat mbili ambazo ni Wilayat ya Shamba ambayo ilichukua Mudiriyat za Makunduchi, Chwaka, Mkokotoni na Bumbwini.Wilayat ya Mjini ilikuwa na Mudiriyat za Mjini na ile ya Magharibi. Pemba yote ilikuwa chini ya Wilayat moja ambayo ilkuwa na Mudiriyat nne za Wete, Konde, Chake Chake na Mkoani.

Mhe. Spika, mamlaka ya kuigawa nchi katika maeneo ya utawala yapo kwa Mhe. Rais wa Zanzibar, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, toleo la 2010, Kifungu cha 2(a). Aidha, Kifungu Nam. 4 (2) cha Sheria Nam. 8 ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 kimetoa mamlaka kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Mapinduzi, kuainisha mipaka ya maeneo ya Tawala za Mikoa na kutaja majina yake.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mwezi Mei mwaka 2015, Mhe. Rais aliigawa nchi kwa kuongeza Wilaya moja kutoka 10 hadi 11 na kufanya marekebisho ya mipaka ya mikoa hasa kule Pemba. Aidha, katika mapitio hayo ya mipaka kumeongezwa pia idadi ya Shehia Unguja na Pemba. Kugawiwa kwa mipaka ya maeneo katika ngazi zote na kuyapa majina mapya ni jambo ambalo linachukuwa muda kufahamika na kuzoeleka miongoni mwa wananchi. Hivyo basi, ilionekana ni busara kuendelea na majina yaliyokuwepo awali ili sio tu kuepuka kuwaparanganya wananchi bali pia hakukuwa na ulazima wa hoja wala haja ya kufanya hivyo kwa wakati ule.

Mhe. Spika, kuhusu lini Serikali itabadilisha majina ya Mikoa yote kwa Wilaya za Unguja na kuwa katika majina ya asili: Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa, hadi hivi sasa Serikali haijawa na mpango wa karibuni wa kubadilisha majina ya Wilaya za Unguja.

Mhe. Yussuf Hassan Idd: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza suali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifutavyo.

a) Kwa kuwa sasa hivi kuna mabadiliko ya kwenda na Sayansi na teknolojia. Je, Serikali haioni ikabadilisha majina haya ili yaendane na wakati.

b) Kwa kuwa baadhi ya mitaa yetu hapa Zanzibar hayatumii majina ya asili, mfano kama Qatar, Uholanzi n.k . Je, Sheria zetu zinasemaje.

Mhe. Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Muwakilishi, kuhusu Serikali kubadili majina ili kuendana na wakati huu wa Sayansi na Teknolojia, nadhani kiufupi kwamba Mheshimiwa, maalezo tumeyasikia na ushauri tumeusikia.

a) Lakini kwa nia njema kabisa naomba kumjibu kwamba kwa sasa hivi hakuna mpango, lakini pale ambapo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo ushauri wake tutauchukua na tutaufanyia kazi.

b) Mhe. Muwakilishi, Sheria zinazohusu au zinazotoa maelekezo kuhusu namna gani mipaka inaweza kufanywa, nirudie kusema kwamba tutaangalia uwezekano na tutafanya mapitio kuona kwamba labda tunaweza kuona utaratibu gani na namna sheria zinavyoelekeza na badala yake tunaweza kuchukua hatua kwa mujibu wa maelekezo au mwelekeo wa sheria inavyotaka jinsi gani tunaweza kufanya.

Mhe. Ali Suleima Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza suala la nyongeza.

Mhe. Spika, katika jamii au katika familia jina la familia linatumika na linaeleweka vizuri, lakini katika baadhi ya mitaa yetu vile vile kuna majina ya asili ambayo yanakuwa rahisi kutambua katika eneo lile, katika suala hili Mheshimiwa, Wilaya zetu za Micheweni, Wete, Mkoani na Chake Chake, unajua unapotaja tu mtu anajua ni wapi.

Je, kwa nini hivi sasa Wizara haichukui hatua labda ya kumshauri Mhe. Rais, umefika wakati wa kufuta majina ya asili, kwa mfano Wilaya ya Makunduchi, Wilaya ya Dunga, Wilaya ya Mfenesini, Wilaya ya Mkokotoni, mimi nafikiria kama ni mifano katika maeneo yetu.

Mhe. Wizara, haioni kuna haja ya kufanya hilo kwa sasa hivi ili kuweka hii historia katika maisha yetu, kwamba Wilaya zinatambulikana kihistoria katika mengineyo.

Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Kwanza nataka nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake ya

awali ya suala mama, baada ya pongezi hizo, naomba nimshukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali, kwa suali lake.

Majina ya mipaka ya maeneo na Wilaya tumeyatangaza mwaka 2015, Wizara yangu ilichukua nafasi hii kwa mujibu wa Sheria Nam.8 ya mwaka 2014, tulimshauri Mhe. Rais kutangaza majina haya na kuongeza Wilaya moja katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

Hata hivyo, nataka nimfahamishe Mhe. Ali Suleiman Ali, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kijitoupele, kwamba suala lake huwa tunalizingatia pale inapokuwa kuna haja ya kufanya kazi hiyo, kwa hivi sasa majina yaliyopo ndio ambayo nimeyatangaza rasmi kwenye Gazeti Rasmi la Serikali, na kwa sasa hivi kama suala mama lilivyoeleza hatujawa na haja ya kubadilisha majina hayo kuyaweka katika majina ya asili kama Mkokotoni, Makunduchi na kwengineko kama ilivyo katika Mikoa ya Pemba.

Kwa hivyo, Unguja tutaendelea kubakia na majina yaliyoko sasa mpaka hapo Serikali itakapoona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo, lakini kwa sasa bado haja hiyo tunaona tutumie majina yanayoonesha kanda zaidi kuliko majina ya asili, na hili tunalifanya kwa sasa kuepuka lile suala la kwamba kila mmoja atataka jina la eneo lake. Mimi nitataka liitwe jina la Mkokotoni, wa Gamba watataka liitwe jina la Gamba.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Ali Suleiman Ali, atustahamilie kwa hili mpaka hapo Serikali itakapoamua kutangaza upya na kuyapitia upya mipaka ya kiutawala, ahsante sana.

Nam. 87

Utumikishaji wa Watoto Katika Maeneo ya Masoko

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:-

Kwa kuwa suala la udhalilishaji limezidi kwa watoto. Na kwa kuwa kumeonekana kuwepo kwa watoto kupewa ajira na kukosa kusoma kwa wakati katika maeneo ya masoko, bandarini, na katika fukwe kwa kupara samaki na usambazaji wa bidhaa.

(a) Je, Serikali haioni watoto wale wanakosa haki yao ya msingi ya elimu.

(b) Ni lini Wizara itatoa elimu kwa jamii ili kutowakosesha watoto haki hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

(a) Mhe. Spika, Naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakari, swali lake namba 87, kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Sheria ya ajira Nam. 11 ya mwaka 2005, kifungu cha sita (6), Ajira zote za watoto pamoja na aina mbaya za ajira kwa watoto zinapigwa marufuku. Hivyo, maafisa husika wa Wizara hufanya ukaguzi kazi maeneo mbali mbali Unguja na Pemba na iwapo wanagundua kuwepo kwa tatizo hili hatua kali za haraka ikiwemo za kisheria huchukuliwa.

Mhe. Spika, Wizara yangu inaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa kupambana Ajira za watoto ambapo imeweza kuhamasisha jamii juu ya kupambana na tatizo la Ajira kwa watoto. Katika baadhi ya maeneo tatizo hilo limepungua na wananchi wanaendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha kuwa watoto hawafanyi kazi na badala yake wanautumia muda huo katika kupata haki zao za msingi ikiwemo elimu. Katika hatua hizo, Wizara imewarejesha skuli watoto 5,085 (Pemba ni 1,953 na Unguja ni 3,132) katika Wilaya 11 walikuwa wanajishughulisha na kazi. Wengi wa watoto hao hivi sasa wanaendelea na masomo yao vizuri.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu inaendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii juu ya suala la kupambana na Ajira za watoto. Katika kila robo mwaka ziara maalumu hufanywa kupita maeneo mbali mbali Unguja na Pemba kuhamasisha jamii kutowaruhusu watoto wao kujishughulisha na ajira na badala yake kujishughulisha zaidi na masomo yao. Pia, vipindi mbali mbali kupitia redio vinatolewa juu ya suala hilo.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Je, Mhe. Waziri, unawaangalia vipi watoto ambao familia zao haziko na wameonekana wakizururа ovyo na kukosa haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Kwa Zanzibar hakuna kesi za watoto ambao wanazururа wasiwe na mtu hata mmoja ama familia, isipokuwa ni nje ya Zanzibar watoto hawa na pia tunawapatia hifadhi ya muda huku tukifanya mawasiliano na Wilaya au eneo husika ili kuwarudisha katika familia zao. Ikitokea Zanzibar kuwa na suala kama hilo basi tunawapatia hifadhi muda huu tukiendelea kutafuta familia zao na tukiwapata tunawapa ushauri na malezi na makuzi bora kwa ajili ya watoto hao.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza suala moja la nyongeza. Katika majibu yake amesema kuna baadhi ya maeneo tatizo hilo limeanza kupungua na wananchi wanashirikiana na Serikali kulimaliza tatizo hizo.

Naomba atueleze ni maeneo gani ambalo tatizo hilo limepungua hadi wananchi kuridhika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Katika maeneo ambayo tumefanikiwa kuwarudisha watoto hao mashuleni kama maeneo yafuatayo:-

Kwa upande wa Unguja ni Nungwi, Mkokotoni, Pwani Mchangani,Kijini Makunduchi, Kendwa, Mwenge Makunduchi, Chumbuni,Mji Mkongwe, Kisauni, Kinuni, Fumba Shakani, Mzuri Makunduchi,Kizimkazi,Tunduni Uzini, Chwaka, Charawe,Marumbi, Kizimkazi Makunduchi, Shaurimoyo, Mchangani, Kiwengwa, Mahonda, Mwanakwerekwe, Jambiyani na Paje.

Kwa upande wa Pemba, Shumba Mjini, Gando, Kojani, Chwaka, Micheweni, Kiuyu Mbuyuni, Tumbe Mashariki, Tumbe Magharini, Ole, Kangani, Mjini Kiuyu, Mjini Ole, Vitongoji, Pujini, Uwandani, Kwale, Wesha, Michungwani, Mkoani Mjini, Majenzi Ndagoni, Wesha, Vitongoji Uwandani, Makoongwe, Muwambe na Wambaa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa heshima kabisa napenda niseme tu kwamba tarehe 23/9/2016 ilikuwa ni Sikukuu ya kuadhimisha elimu bure Zanzibar, na kwa kuwa Mhe. Rais amekuwa akisisitiza sana suala hili la kuwa elimu ni bure, data nzuri zaidi zitaonekana mwaka Januari watakavyoanza kuorodheshwa wanafunzi kuingia madarani nadhani nitakuwa na data nzuri zaidi na zenye uhakika.

Lakini napenda niseme kwamba nampongeza Mhe. Naibu Waziri, wangu kwa jitihada ya majibu aliyoyatoa.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Katika majibu yake amesema kwamba wamefanikiwa kuwarejesha watoto maskuli, mimi naomba aniambie wanafunzi waliorejeshwa wanawake wangapi na wanaume ni wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Jumla ya watoto 2,567 kwa Unguja wamerejeshwa skulini, ambapo kati ya watoto hao 1,082 ni wanawake na 1,485 ni wanaume.

Kwa upande wa Pemba, 2,518 wamerejeshwa skuli ambapo kati ya watoto hao 1,132 ni wanawake na watoto 1,336 ni wanaume.

Nam. 48

Kutopungua Bei ya Nishati ya Mafuta Zanzibar:

(Mhe. Mjumbe, aliyetaka kuuliza suala hili ameliondoa)

Nam. 37

Ugawaji wa Vihori na Tatizo la Bei ya Mwani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imesema mpango wa kugawa VIHORI 500 uko pale pale kwa wakulima wa mwani kama utekelezaji wa kuendeleza zao hilo Zanzibar hayo yamesemwa na Waziri wa Kilimo Julai 23/7/2016, hapo Pwani Mchangani.

a) Je, mpango huo unatarajiwa kutekekelezwa katika kipindi cha muda gani baada ya wakulima kukabiliwa na mazingira magumu katika uvunaji wa zao hilo.

b) Je, Serikali imechukua hatua gani baada ya kuwepo kilio cha muda mrefu cha bei ndogo ya zao hilo wakati Serikali imekiri kuwa zao hilo ni la tatu katika mazao yanayochangia pato la Taifa baada ya kupatikana Bilioni 6.

c) Je, ni lini Serikali itaanza kununua zao hilo kama ilivyo kwa zao la karafuu ili wakulima wake wawe na soko la uhakika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji, Wanawake na Watoto pamoja na Taasisi *ya COSTECH* katika kipindi cha mwaka 2014 ilitoa vihori 100 ambavyo vilikopeshwa kwa wajasiriamali wa mwani katika maeneo tofauti Unguja na Pemba. Hivyo, Serikali inaendelea mpango huo kwa kutafuta utaratibu ambao utawezesha kutekeleza kwa vitendo azma hiyo. Aidha, Serikali imo katika mchakato wa kumaliza mazungumzo na wawekezaji ambao watasaidia kuimarisha hali ya kilimo cha mwani ikiwemo usambazaji wa vihori.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Wizara imechukuwa hatua ili kuongeza bei na kuwapatia tija wakulima wa mwani ikiwa ni pamoja na:-

i. Kuendeleza kutafuta wawekezaji ambao wataweza kuwekeza katika kusarifu mwani hapa Zanzibar ili kuongeza thamani ya mwani.

ii. Kuwahamasisha wakulima kulima mwani mnene aina ya *(cottonii)* ambao una bei nzuri.

iii. Kutafuta na kushajihisha wawekezaji kuanzisha viwanda vya kusindika mwani ili kuongeza thamani na hivyo kuongeza bei na nafasi za ajira.

iv. Kushajihisha matumizi ya mwani kwa binaadamu na wanyama ili kuongeza matumizi ya soko la ndani.

(v) Serikali ina mkakati wa kutoa vifaa vya mwani kwa wakulima ili kuongeza pato lao.

Mhe. Spika, serikali imeandaa Kamati Maalum itakayoshirikisha Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Kamati hiyo inajumuisha wataalamu kutoka Taasisi za serikali ikiwemo taasisi ya Sayansi na Bahari (*IMS*), *COSTECH*, na Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*). Lengo kuu la Kamati hiyo kufanya utafiti yakinifu juu ya kuangalia

uwezekino wa serikali kupitia shirika lake la biashara la Taifa kuweza kununua mwani kama inavyofanywa kwa zao la karafuu. Kamati hiyo tayari imeshaanza kazi za utekelezaji wa majukumu iliyokabidhiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, bahati nzuri leo nina Ilani ya Chama cha Mapinduzi Zanzibar hapa.

1) Vihori 100 mlivyovitoa vimenufaisha wakulima wangapi kwa Unguja na Pemba na umesema vihori 100 mlivyotoa kukopesha wajasiriamali, ni shilingi ngapi mlivyokuwa mnavikopesha. Maana yake itabidi nizungumze kidogo kidogo ili Naibu Waziri, apate kunisikia asije akapata kigugumizi wakati wa kujibu.

2) Mhe. Spika, nina Ilani ya Chama cha Mapinduzi hapa ukurasa wa 134, naona watu hawa jinsi wanavyoteseka kutafuta...

Mhe. Spika: Uliza swali Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mipango hii mliyoieleza itachukua muda gani utekelezaji wake baada ya wakulima wa mwani kuwa na matatizo mengi kwa miaka mingi likiwemo tatizo la vifaa vya kutendea kazi na hasa walioniajiri miye wakanileta humu ndani ikiwemo Michamvi, Muungoni, Paje, Jambiani na Bwejuu, lini watanufaika na vifaa hivi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa swali lake la nyongeza.

a) Mheshimiwa, ametaka kujua ni shilingi ngapi zimetumika na vile vile alitaka kujua ni wakulima wangapi wamefaidika. Kwa jibu sahihi na zuri kabisa nitaomba kumjibu kwa mandishi.

b) Mpango huu utatekelezwa pale serikali itakapokamilisha azma yake. Vile vile, masuala haya yanaendana na bajeti, kwa hivyo, nitaomba atuachie mpaka mwaka wa fedha ujao basi tutaweza kulitekeleza na kulisimamia suala hili la vihori.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Spika, mara nyingi viongozi wetu wote sio wa Wizara ya Kilimo tu, wanakuwa na masuala mengi wanayohojiwa, wanayoyaahidi kuhusu mwani. Mimi nataka kuwauliza na hii itakuwa ni mara ya tatu, niliwahi kumuuliza Mhe. Waziri wa Biashara hapa hapa sikupata jibu, nikamuuliza Mhe. Waziri wa Kilimo sikupata jibu, Mhe. Waziri wa Fedha,

hapa kidogo akajibu. Ninachotaka kumuuliza tupewe faida ya mwani au gharama za mwani kwa heka, zinapimika ijapokuwa ipo ndani ya maji, ili tujuwe una faida ama hauna faida, kuliko kila siku tunawaahidi watu vitu ambavyo haviwezekani. Kama itakuwa vina faida au havina faida wananchi wajuwe ili watafute kilimo chengine. Kwa hivyo, naomba gharama za heka moja, ama hekta moja ya mwani na faida yake.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu mazuri aliyoyatoa.

Mhe. Spika, serikali imejitahidi sana kutoa majibu sahihi. Suala la mwani ni suala ambalo lazima tuiunge mkono serikali, wananchi. Ni zao peke yake ambalo limeajiri watu wengi, hakuna kiwanda chochote ambacho kimeajiri idadi ya watu wengi kama hao. Hiyo nikuonesha kwamba ni zao ambalo linamsukumo mkubwa. Ni zao peke yake ambalo unaweza kuvuna mara sita kwa mwaka, hakuna zao lolote jengine ambalo unaweza kuvuna, ni zao la tatu ambalo linachangia *GDP* ya Zanzibar. Hivyo, ni kuonesha wazi kwamba ni zao muhimu.

Lakini hata zao ambalo tunalitegemea la karafuu ambalo bei zake za duniani kila siku zinabadilika na lenyewe linakutwa na msukosuko. Hata utalii ambao niwakwanza katika uchumi na wenyewe hukumbwa na misukosuko na bei zikashuka. Leo zao la mwani limekubwa na msukosuko wa bei kutokana wenzetu ambao wanazalisha mwani kama Indonesia wanazalisha tani sita, Philipins wanazalisha tani laki nane, wao wanaweza ku-*control* bei ya mwani wanavyotaka. Ndio maana serikali inamshukuru sana Mhe. Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kuchukua juhudi ya kuzungumza na *UNIDO* kwamba waanze kujenga kiwanda Pemba ambacho kitasaidia kukata mwani na hatimae bei za mwani kuwa za juu.

Mhe. Spika, hivi sasa tuna wawekezaji wapo tayari kuzungumza nao waweke kiwanda chengine hapa Zanzibar ambacho nacho chenyewe kitakata mwani. Matumizi ya mwani yapo 17 Ukianzia chakula na keki za mwani, kuna sabuni za mwani. Mimi mwenyewe Mheshimiwa, nilikuwa nina tatizo kubwa sana la mba kichwani kuanzia sasa nakogea sabuni ya mwani na nimetokana na tatizo hilo. Kwanza ninachowaomba wananchi wajifunze matumizi ya mwani, mwani ni chakula, mwani na mbolea, mwani ni dawa. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Ali Sleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, mimi naipongeza serikali kwa nia njema kabisa ya kuhakikisha kwamba, wakulima wetu wa zao la mwani wanapata ajira na kupata maslahi ya maisha yao. Lakini linalozungumzwa hapa kubwa ambalo ni kero kwao, ni utaratibu mzima wa bei ambayo iko chini kabisa haistahiki na kazi zao.

Je, kwa kuwa Mheshimiwa katika jibu mama alisema tu kwamba pana utaratibu ambao umepangwa sasa hivi wa kuanzishwa viwanda ambavyo viwanda hivyo malighafi zitatokana na hapa hapa kwetu, itakuwa rasilimali ile ina bei zaidi. Ni sehemu gani ambazo zimeangaliwa katika ujenzi wa viwanda hivyo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza kwa mujibu wa utafiti waliofanya wenzetu wa *UNIDO* nimeona sehemu ya Wilaya ya Micheweni ambapo ndio kunazalishwa mwani kwa wingi wataanza na hichi kiwanda kidogo ambacho kinajengwa, nimeshawakaguza kwenye *site* wameangalia sehemu ya Makangale na wameridhika napo, tusubiri tu na ameshirikiana na mmoja kati ya wanaonunua mwani hapa Zanzibara ili kuwa *private sector* pamoja na kuwa na yeye pamoja.

Kwa hivyo, hapo ni pahali pa kwanza, pahali pa pili ambapo tunategemea kujenga ni pahali ambapo muwekezaji baada ya kumkaguza atatwambia, tuna maeneo mengi lakini sisemi hivi sasa mpaka muwekezaji atakapokuja aridhike kutokana na *infrastructures* zilizopo ndio tutamwambia. Lakini nakuhakikishia kabisa ni maeneo ambayo wakulima wa mwani wanazalisha mwani kwa wingi, kwa sababu hatutaki kuingia gharama za usafirishaji, kutoka sehemu ya uzalishaji na mahali ambapo patawekwa kiwanda.

Kwa hivyo, namuhakikishia asiwe na wasi wasi na Wajumbe wa Baraza tutawaarifu rasmi, watakwenda watakagua na wataona shughuli itakayofanyika, watupe muda tu, tunalishughulikia.

Nam. 108

Marejesho ya Madeni kwa Wakulima wa Karafuu

Mhe. Mussa Foum Mussa: Aliuliza:-
Katika kipindi cha mwaka 2014 – 2015 serikali imetoa mikopo yenye thamani ya TZS millioni 342.3 kwa wakulima 126 wa karafuu wa Unguja na Pemba.

(a) Je, kiasi gani mpaka sasa kilichorejeshwa.

(b) Je, huko nyuma hakuna wakulima wengine wanaodaiwa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Alijibu:-
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 108 kama ifuatavyo lenye vipengele (a) na (b) kama linavyoulizwa.
Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa ufafanuzi kuwa mkopo wa TZS 342.3 milioni ulitolewa kwa wakulima 126 wa Karafuu wa Unguja na Pemba ulitolewa mwaka 2015/2016 na sio mwaka 2014/2015 kama swali lilivyoulizwa.

(a) Katika kipindi cha 2015/2016, serikali ilikopesha wakulima 126, kati ya hapo 43 kutoka Unguja na 83 kutoka Pemba. Kiasi cha fedha zilizokopeshwa kwa wakulima ni TZS 3423 milioni na wamefanikiwa kulipa kiasi cha 329,1 milioni na kilichobaki ni TZS.13.1 milioni.

(b) Ni kweli katika mikopo iliyotolewa huko nyuma wakulima wanadaiwa Jumla ya deni ya TZS6.2 milioni kwa kipindi cha 2013/2014 na 2014/2015. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 wakulima kutoka Pemba wanadaiwa TZS.2.4 milioni na Unguja ni TZS. 2.1 milion. Jumla ya deni kwa 2013/2014 ni TZS. 4.5 milioni. Kwa mwaka 2014/2013 wakulima kutoka Pemba wanadaiwa TZS. 1.7 milioni.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, sasa inasemekana kwamba kuna wakulima wa karafuu kutoka Morogoro Tanzania Bara wanaziuza karafuu hizo hapa hapa Zanzibar na inapelekea kuharibika kwa karafuu zetu za Zanzibar katika soko la ulimwengu.

Je, suala hili ni kweli na ikiwa ni kweli Mhe. Waziri, hivi sasa Zanzibar ipo Sheria ya kudhibiti uingizwaji wa karafuu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, swali lake ni jipya kwa sababu swali la msingi ni mikopo, lakini kama majibu unayo Mhe. Waziri, unaweza kumjibu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, swali la nyongeza la Mhe. Mussa, naomba nimjibu kama ifuatavyo:

Ni kweli zilikamatwa karafuu kutoka Morogoro na kutoka Tanga, karafuu hizi ziliingia kwa utaratibu wa magendo na kwa hila, kwa sababu walitaka wazichanganye ili kupewa bei kama karafuu za Zanzibar. Kwa mujibu wa

sheria tuliyokuwa nayo mpaka sasa hivi haijazungumza chochote kuhusu karafuu zilizoingizwa kutoka nje, kwa sababu wakati ule karafuu zinazotoka Bara hazikuwa nyingi ya hivyo. Lakini Wizara imekaa na kutafakari na inaangalia utaratibu mzuri wa kuona kwamba hizi karafuu zinazotoka Bara na sio karafuu tu bali kuna viungo vingi sasa hivi vinatoka Bara vikiwa katika utaratibu mzuri na kununuliwa na Shirika letu la *ZSTC* kwa taratibu maalum zinazofuata sheria.

Mhe. Spika: Napenda niwakumbushe swali la msingi ni swali la Mikopo.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, katika kuwasaidia wakulima, serikali inatoa mikopo kwa wazalishaji wa karafuu, hata hivyo kwa muda mrefu wizara ya biashara tangu bajeti ya mwaka 2012/13 imekuwa ikielezea dhamira yake ya kuwa na *brand* kwenye karafuu zetu ili kulinda uchakachuaji wa karafuu kutoka nchi jirani. Je, ni lini Wizara itatimiza dhamira yake hiyo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Machono, swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Suala la *branding* ni jambo la kitaalamu, halifanyi mtu akajitangazia kama hii ni *brand* yangu. Na ni kweli kwamba kipindi cha kwamba miaka mitatu serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilikuwa ikifuatilia utaratibu wa kui-*brand* karafuu ya Zanzibar. Naomba niseme kwamba hatua ya kwanza ya utaratibu huu wa kui-*brand* karafuu ya Zanzibar umeshakamilika na tumeshauriwa tusifanye tu *brand* ya karafuu peke yake. Lakini katika *brand* imeongezwa kitu kama pilipili manga, pilipili hoho pamoja na mdalasini, na karafuu na imeshapewa jina *brand* yetu na hivi sasa hivi tupo katika mchakato wa kusajili hii *brand* inaitwa *'Zanzibar Exhotic Original'*. Tumepanga kwamba Mhe. Rais' katika Sherehe za Mapinduzi ndio aje afungue rasmi hii sehemu ya kwanza ya *brand*.

Mhe. Spika, sehemu ya pili, kinachotakiwa sasa hivi, tunatakiwa tupate maelezo ya kisayansi juu ya sifa za karafuu za Zanzibar. Kwa bahati mbaya vyombo vyetu vinavyotengeneza vya ubora kwa mfano kama cha Zanzibar na cha Bara walikuwa hawana uwezo wa kufanya shughuli hii ya kutoa maelezo ya kisayansi kwa mazao ya viungo. Kama mnavyojua mazao ya viungo Afrika nzima vinazalishwa Tanzania, Comoro na Madagasca. Kwa hivyo, sasa hivi tunatafuta kampuni ya *standard* iliyopo India ambayo ndiyo wanaouzoefu wa kutoa maelezo ya kitaalamu juu ya mazao ya viungo kwa kushirikiana na bodi yetu ya Zanzibar ya Ubora ili watupe taarifa rasmi ambazo tutazitumia katika maelezo ya karafuu au bidhaa nilizozisema ambazo ni karafuu, mdalasini, pilipili manga na pilipili hoho. Kazi hiyo itakapokamilika itakuwa tumeshakamilisha zoezi zima la hii kazi ya *branding*.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye vipengele (a) na (b). Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, napenda kuuliza mikopo hii hutolewa kwa lengo la kuwasaidia wakulima wenye mashamba kwa kuhudumia mashamba yao kabla ya ule muda kuvuna. Na kwa sababu huwa kuna tatizo la kujitokeza watu wanaoomba mikopo ambao hawana mashamba ya mikarafuu.

a) Je, Wizara ya Biashara kwa kupitia Shirika lake la *ZSTC* wanatumia kigezo gani kuhakikisha kwamba mikopo wanayoitoa ni kwa wale wenye mashamba tu na sio kwa watu wengine ambao wanajitokeza kuomba mikopo wakati wa uchumaji.

b) Je, Serikali haioni kutoa mikopo hiyo wakati wa kuchuma karafuu sio muda muwafaka na badala yake ingekuwa ni vyema pesa hizo zikakopeshwa wakulima wakati wa masika wakaweza kupanda mikarafuu na kuongeza zao letu, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa kama hivi ifuatavyo:

a) Kwanza kuhusu vigezo vinavyotumika kuwapa wakulima mikopo, mkulima hapewi tu mkopo bila ya kufatiliwa na kuna kazi inabidi ifanywe, kuna masheha wanashirikishwa, lakini pia huyo anayechukua mkopo inabidi adhaminiwe. Kwa hivyo, anapokuwa na mchakato mzima huu ndio unaomfanya kumuhakikishia kama huyo anaekopa ni mtu ambaye kweli anayo mashamba ya karafuu, anafatiliwa kwa mchakato ambao umewekwa na *ZSTC.*

b) Kuhusu mikopo kwa ajili ya mvua ili kupanda miche. Lazima niseme kwamba miche huwa wanapewa bura na serikali. Hii mikopo wanayopewa kwa ajili ya kujiandaa kwa ajili ya uchumaji na kukausha na kufanya kazi zote zile ambazo zinatakiwe zifanywe wakati wa uvunaji wa karafuu. Kwa sasa hivi tunaona kile ambacho muhimu zaidi ni ule wakati wa uvunaji wa karafuu ambao unapatiwa mkopo mapema kidogo ili wajitayarishe. Lakini kwa upande wa upandaji miche kama nilivyosema serikali inawahudumia inawapa miche bure na wao wanatakiwa miche ile waisimamie. Kwa hivyo, tutaendelea kuwa na utaratibu huo mpaka hapo tutakapofanya utaratibu mzima wa kuangalia hii sekta ya karafuu ilivyo

Nam. 109

Tatizo la Kuendelea kwa Biashara za Serikali

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Aliuliza:-

Serikali hufanya vyanzo vya biashara ili kutoa huduma kwa wananchi wake au kupata mapato na manufaa ya watu wote, la kushangaza ni kwamba biashara hizo hufa au hufilisika na biashara hiyo hiyo hupewa mfanyabiashara binafsi na biashara hiyo huimarika na kumnufaisha kwa kiasi kikubwa.

a) Je, kwa nini miradi ya biashara inayosimamiwa na serikali huwa haifanyi vizuri zaidi ukilinganisha na anapopewa mtu binafsi.

b) Nini adhabu ya waliohusika kuleta hasara serikali na kuikosesha mapato.
c) Serikali imejipanga vipi kurudisha biashara zake kama zamani ili kudhibiti biashara ambazo ni nguzo ya Serikali.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Alijibu:-
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 109 kama lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, moja ya kazi kubwa ya serikali ni pamoja na kuwezesha utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi wake kwa kadri hali ya uwezo wa serikali unavyoruhusu, hivyo, huanzishwa vitega uchumi vya kibiashara kwa lengo hilo. Hivyo, ni muhimu kuelewa kwamba ipo tofauti kubwa kati ya biashara zinazomilikiwa na mtu binafsi na zile zinazosimamiwa na serikali kwani hizo za serikali huanzishwa kwa sababu maalum.

Mhe. Spika, biashara zinazomilikiwa na watu binafsi lengo lake kubwa ni kujikita kwenye faida kubwa zaidi kuliko hata wakati mwengine kuhudumia wananchi.

Mhe. Spika, biashara nyingi ambazo zinasimamiwa na Serikali ni zile ambazo zinatoa huduma muhimu kwa wananchi na kama inavyoeleweka wakati mwengine Serikali inalazimika kusaidia gharama za uendeshaji kwenye taasisi hizo kwa lengo la kuwawezesha wananchi kupata huduma hizo kwa unafuu, mfano mzuri ni kama Shirika la Umeme na Mamlaka ya Maji na Mashirika mengine yaliyopo. Hivyo, uwezekano wa kutofanya vizuri kwa taasisi kama

hizo ni mkubwa zaidi kulinganisha na zile zinazomilikiwa na watu binafsi.

(b) Shughuli zote za Serikali zinasimamiwa na sheria na Kanuni za Taasisi inayohusika. Kwa msingi huo, maofisa na watendaji ambao husababisha hasara kwa Serikali huchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria na kanuni zilizopo.

(c) Serikali haina lengo la kujiingiza tena katika kufanya biashara za bidhaa mbali kama ilivyokuwa zamani, ila itaendelea na jukumu la kuhamasisha na kuimarisha biashara kwa kuweka sera, sheria na kanuni zitakazojenga mazingira bora ya biashara, na uwekezaji. Pia, itaweka na kusimamia mazingara yatakayoirahisishia sekta binafsi ufanyaji wa kazi kwa urahisi na ufanisi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, ninamshukuru sana Mhe. Waziri, kwa majibu yake mazuri lakini nilikuwa ninamuuliza Mhe. Waziri kwamba, kwa kutokuwa ni sahihi lakini ni maneno tu ya kawaida ambayo atanisahihisha Waziri kwamba suala la sukari, mchele na unga katika Serikali zetu za awamu ya kwanza ilikuwa ni kitu ambacho biashara hii alikuwa hairuhusiwi kuchukua mtu mwengine yeyote zaidi ya Serikali ili kuhakikisha wananchi wake wanapata chakula hiki kwa uhakika na kwa shughuli zote. Sasa hili sijui kwanza ilikuwa ni kweli au si kweli. Lakini kama ni kweli haioni umuhimu wa kurudisha tena suala la sukari, mchele na unga kuwa ni sekta ya Serikali.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba sasa hivi Serikali haijiingizi tena kufanya biashara kama hivi. Huko nyuma Serikali ilikuwa inafanya biashara zote sio tu sukari, mchele na unga wa ngano, lakini vitu vyote kulikuwa na maduka ya Serikali na kulikuwa na Shirika la Biashara likifanya mambo hayo na Shirika lenyewe lilikuwa BIZANJE ambao likinunua vyakula, sukari, mchele na unga wa ngano.

Lakini Mhe. Spika, kwa wakati ule Shirika hili lilipata hasara kubwa sana na mwisho wake Shirika likabidi lifungwe kiserikali. Mazingira ya sasa hivi ya biashara huria ambayo tumewaachia wafanyabiashara binafsi ambao wana uwezo kabisa na wanaweza kuhimili matatizo ya bei kupanda na bei kushuka na vile vile upungufu wa faida, wao wafanyabiashara binafsi wataweza kuhimili hivyo na kuhimili vile vile suala zima la ushindani wa kibiashara. Nadhani Serikali si busara kuingia katika biashara hii ya mchele, sukari na unga wa ngano.

Lakini nini Serikali inafanya sasa hivi, inasimamia kwa kuweka bei elekevu, lakini vile vile kufatilia kwamba vyakula hivi hutolewa kwa mujibu wa viwango na ubora unaostahiki kwa binaadamu kuvitumia.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Awali ya yote nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kwa majibu yake mazuri katika swali hilo.Pamoja na hayo naomba kuuliza kama ifuatavyo. Serikali iliacha kufanya biashara kuanzia miaka ya mwisho ya 1990 kutokana na mabadiliko ya kiuchumi duniani. Lakini kabla ya hapo Wizara ya Biashara ilikuwa na BIZANJE, Shirika la Viwanda vya Serikali, Shirika la Magari na Taasisi nyingi. Swali langu liko hapa, je, zile mali ambazo zilikuwa zikimilikiwa na mashirika haya mfano Shirika la Viwanda walikuwa na viwanda kama 11 maeneo mbali mbali, pamoja na maghala na mali nyengine na BIZANJE na juzi juzi tu Shirika la Magari nalo lilikuwa na jengo ambalo linatumiwa na Benki ya Posta, *NMB* na *PBZ* Malindi. Hizi mali zimerudi Serikali Kuu au ziko Wizara ya Biashara. Je, Serikali haoni kwamba kuna haja ya kufanya uhakiki kwa kupitia Tume Maalum kuzijua mali hizi ziko wapi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ni kweli katika miaka 1990, kwa sababu ya hali halisi ya mazingira ya kiuchumi na kibiashara katika ulimwengu mzima Serikali ya Mapinduzi nayo ilibidi nayo vile vile ibinafsishe baadhi ya haya Mashirika ya Serikali. Kuhusu Mali za Mashirika haya Mhe. Machano, atakuwa anaelewa kwamba mali hizi ziliuzwa kipindi cha miaka 1990, mwishoni na mwaka 2000, 2005, 2010, mali hizi zimeuzwa nyengine, nyengine zimebakishwa Wizara ya Fedha zinakodishwa, nyengine zimebakishwa, kama maghala yamebakishwa Wizara ya Biashara na yameshakodishwa miaka mingi, mpaka sasa hivi mengi yapo kwenye mikono ya watu binafsi.

Kuhusu nyumba iliyokuwa Shirika la Magari, nyumba ile Benki ya Posta bado nadhani iko Wizara ya Fedha iko kwenye mikono ya Serikali na nyumba iliyokuwa *PBZ* sasa hivi nyumba ile imerudishwa katika mikono ya Wizara ya Biashara baada ya kubadilishana na nyumba iliyokuwa ya *motor sale* ambayo ndio imepewa *PBZ* kujenga makao makuu ya tawi lake pale. Lakini kama nilivyosema kwa miaka yote ya nyuma huko hizi mali zimebadilishwa zimeuzwa nyengine, nyengine zimepelekwa Serikalini, nyengine mpaka sasa hivi zimekodishwa kwa muda mrefu. Ahsante.

Nam. 13

Kuanzishwa kwa Kigoda cha Sultan Qabus

(Mheshimiwa Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 25

Kuimarishwa kwa Elimu ya Watu Wazima

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Aliuliza:-

Lengo kuu la mfumo wa Elimu kwa wote na kuweka utaratibu wa elimu bila ya malipo ni kuwapatia elimu muhimu wananchi wote ili kuwasaidia katika maisha yao.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwahamasisha na kuimarisha elimu ya watu wazima na vipi inawashirikisha katika masuala ya matamasha na maadhimisho mbali mbali ya elimu ili na wao wajione kuwa ni sehemu ya wanafunzi wanaoshirikishwa katika shughuli hizo.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuzisaidia familia maskini sana katika kuhakikisha kuwa na wao, hususan, watoto wao wanapatiwa elimu ili iwakomboe na janga hili la umasikini.

(c) Je, ni watu wazima wangapi wameendelezwa na Wizara hadi kufikia viwango vya *Degree*.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba nimuombe muuliza maswali suala hili aliondoe kwani lilijibiwa juzi likiwa na namba 92.

Mhe. Spika: Samahani, unaliondosha swali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Namuomba muuliza maswali aliondoe kwa sababu swali hili lilijibiwa juzi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, swali lako lilijibiwa juzi.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii swali langu kwa kweli linalingana na lile lilotoka tarehe 23/11/2016.

Mhe. Spika: Lilikuwa ni swali lako au?

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Tarehe 23/11/2016, lakini lile la tarehe 23/11/2016 lilikuwa ni swali linahusu *overview* ya hata ukiisoma hapa unaona tofauti ipo. Sasa mimi nilitaka nijibiwe hili kwa ile mikakati ambayo imepangwa. Nitatoa mfano namna ninavyotaka lijibiwe.

Mhe. Spika: Basi Mheshimiwa. Mhe. Naibu Waziri, naomba ulijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Dkt. Makame Ali Ussi, Mwakilishi wa Jimbo la Mtopepo swali lake nambari 25 lenye sehemu (a), (b) na (c). Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza Elimu bila Malipo kwa watu wote wakiwemo watoto na watu wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu.Tokea wakati huo, elimu ya watu wazima imekuwa ikitolewa katika vituo mbali mbali vikiwemo sehemu za kazi, kambi za wavuvi na skuli mbali mbali zilioko katika maeneo yanayoishi watu. Kutokana na mwitikio mzuri wa wananchi na kutokana na watoto wengi kujiunga na elimu ya lazima, asilimia ya watu wanaojua kusoma na kuandika wenye umri kuanzia miaka 15 na kuendelea imeongezeka sana. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, asilimia ya wakaazi wa Zanzibar wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu imefikia asilimia 83.4. Baada ua maelezo hayo, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wizara imewahamasisha watu wazima wasiojua kusoma na kuandika kujiunga na madarasa ya kisomo kwa kutumia vipindi vya Redio na Televisheni. Pia, wizara imeandaa mikutano na viongozi na watendaji mbali mbali wa mikoa, wilaya, shehia na walimu wakuu kuhamasisha ufunguaji wa madarasa mapya ya kisomo cha watu wazima. Aidha, Tamasha la Juma la Elimu ya Watu wazima huadhimishwa kitaifa na kimataifa kila mwaka kuanzia tarehe 1 hadi 8 Septemba. Kwa mwaka huu, kilele cha Tamasha liliadhimishwa kitaifa huko Mwambe Mkoa wa Kusini, Pemba tarehe 8 Septemba na liliwashirikisha wanakisoma kikamilifu.

(b) Serikali ya Mapinduzi imewapunguzia wananchi wa kipato cha chini gharama za elimu kwa watoto wao kwa kufuta michango ya wanafunzi katika skuli zote za maandalizi na msingi za Serikali. Serikali imezipatia skuli zote za maandalizi na msingi chaki na madaftari ya kuandikia kwa wanafunzi wote. Pia, skuli zote zimepatiwa Shs. 500,000/= kwa ajili ya gharama za matengenezo madogo madogo au malipo ya umeme na maji. Kwa upande wa skuli za Sekondari, Serikali imechukuwa jukumu la kulipia ada za mitihani kuanzia Mitihani ya kidato cha Pili, Kidato cha nne na Kidato cha Sita. Hatua hizo zote zimesaidia sana katika kuwawezesha wanafunzi kutoka familia masikini kupata elimu bora. Vile vile, wanafunzi walioacha masomo njiani, wanahamasishwa kurudia tena masomo yao kwa kujiunga na vituo vya Elimu Mbadala au madarasa ya elimu mbadala.

(c) Watu wazima wengi wanaojiendeleza kimasomo, lakini Wizara haina kumbukumbu ya watu wazima waliopitia madarasa ya kisomo cha kufuta ujinga na kutojua kusoma na kuandika na wakajiendeleza na hatimae wakahitimu masomo ya ngazi ya Shahada ya kwanza. Hata hivyo, wapo watu wazima wanaojiendeleza katika fani mbali mbali na kufaulu na kutunukiwa vyeti, Stashada na hata Shahada kama vile Fani ya Sheria, Ualimu, Uongozi na Utawala, Uhasibu, Uchumi na kadhalika. Napenda kutoa wito kwa wananchi wajiendeleze kwa njia mbali mbali ikiwemo kupitia masomo yanayoendeshwa na Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo ya Fani ya Sheria na kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambacho kina matawi yake Unguja na Pemba. Masomo yanaendeshwa kwa utaratibu unaomwezesha mwanafunzi kusoma kwa wakati wake bila ya kuathiri shughuli zake za kazi. Wahenga walisema 'Elimu haina mwisho'.

Mhe. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Spika, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri sana na ndio ilivyokuwa nimetegemea. Lakini pia nilitaka ufafanuzi zaidi hapa kwamba kuna vituo maalum vya kufundishia watu wazima, yaani Vituo vya Elimu ya Watu Wazima. Sasa nauliza kwa sababu mimi nishakuwa huko Mikoani ninajua jinsi gani hii Elimu ya Watu Wazima inavyokwenda. Sasa nilikuwa nauliza tu hivi vituo vilivyowekwa vya Elimu kwa Watu Wazima vinakidhi viwango vya kutoa elimu kwa Watu Wazima? Maana yake utakuta wengine hawana pahala maalum wanakaa mahala wanafundisha. Sasa ninataka kujua kuna vituo maalum ambavyo mmeviweka na ambavyo mna viratibu vituo hivyo kwa utaratibu maalum ili kuimarisha hii elimu ya watu wazima.

La pili, nilitaka kujua walimu namna mnawa-*coordinate* wale walimu na kuwafatilia kwa sifa kwa sababu tunajua kwa wale ni wanafunzi tunajua kwamba watasoma sayansi na kuna watakaosoma *Art.* Je, kuna walimu wa Sayansi na *Art* wanaofundisha katika sehemu za walimu wa watu wazima.

Halafu nilitaka kujua usimamizi *supervision* kwa walimu, walimu hawa wanaosomesha watu wazima.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, maswali mawili tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Spika, ni kwamba vituo hivi vya kisomo vinasimamiwa ipasavyo na Idara inayohusika na Elimu ya Watu Wazima, vinaratibiwa na vinajulikana mpaka idadi yake.

b) Ni kwamba walimu wanaosomesha katika vituo hivi ni walimu ambao wanajitolea, lakini wanasimamiwa na Mwalimu Mkuu wa Skuli iliyopo katika shehia ambapo kituo hicho kipo, huo ndio utaratibu ambao tunafanya kwa sasa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, mzee wetu marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Mungu amlaze pahala pema peponi, alisema tu kwamba watu watafuta ujinga wa kusoma na kuandika kwa njia yoyote na hapo ndio ikaanzishwa Elimu ya Watu Wazima. Lakini leo tuna miaka kama 52, hivyo, ni eneo gani ambalo mpaka sasa hivi liko nyuma kabisa kwa watu wake ambao hawajui kusoma na kuandika katika Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, mpaka sasa hatujafanya utafiti wa kimaeneo kuonesha eneo gani liko nyuma na eneo gani liko mbele zaidi. Lakini tutapofanya utafiti huo basi utajua taarifa sahihi. Sasa hivi utafiti tuliofanya ni kujua tu idadi ya watu wanaojua kusoma Zanzibar, lakini umetukumbusha na *inshaallah* tutafanya utafiti huo na tutajua eneo gani zaidi liko nyuma.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani swali moja la nyongeza. Kwa kuwa walimu wanaofundisha watu wazima wanakabiliwa na mazingira magumu sana ya ufundishaji kuliko hata walimu wa shule. Hata hivyo, wanafanya kizalendo. Je, Wizara yako ina mpango gani ya kuwaongezea posho lao hawa walimu angalau likafikia shilingi hamsini elfu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, hivi karibuni nimekuwa na ziara ya kutembelea vituo hivi vya kusoma na ni kweli walimu wanaosomesha katika vituo hivi walitaja changamoto nyingi, lakini moja ni hii posho. Sasa Wizara yangu ni kuwa hivi sasa inajaribu kuyapitia maposho yote yanayotolewa kwa wafanyakazi katika Wizara hii na *inshaallah* pengine itakapokamilika matokeo tutapata kuyaona. Kwa kweli hatuangalii maposho ya wanaosomesha elimu ya watu wazima peke yao, lakini mfumo mzima wa maposho katika Wizara ya Elimu tunaufanyia kazi hivi sasa. Ahsante.

Nam. 63

Gharama za Ujenzi wa Barabara ya Fuoni – Tunguu

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:-
Ni kiasi gani cha fedha kimepangiwa katika ujenzi wa barabara ya Fuoni kwenda Tunguu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Tunguu swali lake Nam. 63 kama ifuatavyo:-

Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Mwanakwerekwe/Tunguu una urefu wa kilomita 12.6 unajegwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kwa kiwango cha lami na unajengwa kwa awamu.

Mradi huu umekusudia kujenga barabara mbili ambazo zitajumuisha sehemu za waendao kwa miguu, wapanda baskeli, eneo la kugawa barabara ambalo siku za baadae litawekewa taa (*street light*), eneo la mitaro na eneo la kupanda miti.

Katika awamu ya kwanza barabara hiyo tayari imeshajengwa kilomita nne (4*km*) kuanzia Mwanakwerekwe Makaburini hadi Kituo cha Polisi Fuoni kwa kiwango cha lami. Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na awamu nyengine, hivyo kwa sasa bado hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Fuoni kwenda Tunguu.

Ujenzi wa barabara hiyo utaanza mara tu fedha za kutosha zitakapopatikana. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi): Ahsante Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa kujibu maswali kwa umakini zaidi. Mhe. Spika, wakati unajengwa ujenzi wa barabara kutoka Mwanakwerekwe/Fuoni wananchi wengi walipata changamoto nyingi na hasa kusababisha pia miili yao wakati wa kusafiri kutoka Mkoa wa Kusini kuja Mjini kupata huduma tofauti wameanza kuwa kama wanapepesuka pepesuka kama wanataka kupungwa, maana yake magari yalikuwa yanatikisika.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri, una mpango gani kwa hawa wananchi ambao wamepata tabu kidogo katika ujenzi wa barabara hizi kupata kikohozi, maana yake tulikuwa tunazungumza nao mara wanakuwa kama wanatikisika tikisika hivi labda watapelekwa India kwa matibabu kutokana na afya zao zilivyoathirika.

b) Katika ujenzi ambao uliopangwa kutoka Fuoni kwenda Tunguu baada ya changamoto iliyojitokeza katika barabara ya Fuoni/Mwanakwerekwe kutokana na hali ya vumbi, lakini katika eneo la Tunguu kuna vyuo vikuu na huduma ambazo wananchi wanapata kama polisi, ofisi ya Mkoa. Je, utahakikisha vipi kuwa hizi athari zilizojitokeza katika maeneo haya hayatajirudia baada yale yaliyotokezea katika barabara ya Fuoni. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ni kweli kama nilivyosema hapo kabla kwamba sisi vile vile tulikuwa tunaumia sana kwa sababu pia na sisi tulikuwa ni watumiaji wa ile barabara kutokana na kuathirika kwa vumbi lilokuwepo kwa wakati ule. Lakini kama tujuavyo kwamba maendeleo yote yanakuwa na changamoto zake na hizi changamoto za kiafya kusema kweli ni changamoto ambazo tunawashukuru sana wananchi wameweza kuzikubali na baadae wakawa wastahamilivu hadi ile barabara ilipomalizika na hivi sasa wanafaidi matunda ya subra yao waliyoionesha katika barabara ile.
Kuhusu suala jengine tunamuhakikishia kwamba kawaida katika utengenezaji wa barabara iwapo kutatokezea kuharibika kwa barabara basi kwa majengo yote yale sisi tunaomba wale ambao wamehisi nyumba zao zimepata athari yoyote wakati wa ujenzi huu walete malalamiko yao na sisi tutayafanyia kazi na itapothibitika kama kweli basi hatua ipasavyo tutachukua kuhakikisha tunalipa hizo fidia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwa kuwa Wizara ya Mawasiliano kwa kawaida hutenga fungu maalum kwa ajili ya kutoa fidia kwa wale wanaoathirika. Je, ni kwa nini Wizara hii ya Mawasiliano haikutenga fungu hilo kwa wale watakaoathirika kwa ajili ya kulipa fidia kutokana na ujenzi wa barabara ya Mwanakwerekwe/Fuoni.

b) Na kama lipo hilo fungu, je, ni lini wale wanaostahiki watalipwa fidia hiyo. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, swali hili niliwahi kuuliza hapo kabla nikasema kwamba, barabara hii ya kuanzia Mwanakwerekwe Makaburini mpaka Fuoni pale tulipofika hatujalipa fidia ya aina yoyote. Hatukulipa fidia kwa sababu ile ilikuwa katika ramani ya mipangomiji tokea kipindi cha 1999 kwamba, ile itakuwa ni hifadhi ya barabara na sisi hifadhi yetu ya barabara ni mita 15. Kwa hiyo, nataka kumwambia kwamba wale ambao wanastahiki fidia katika barabara ile hamna, kwa hiyo, hakuna kusema tutalipa lini. Isipokuwa kama kumetokea athari wakati tunajenga barabara basi tutaangalia utaratibu athari hizo zimetokana na kwamba zile nyumba zimetikisika, au athari hiyo ni ya aina gani. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi kwa dhati kabisa naipongeza serikali yetu hii chini ya Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuangalia ubora na maendeleo kwa wananchi wake katika maeneo mbali mbali sehemu ya usafiri, afya, maji na mambo mengineyo.

Kwa kuwa barabara ya Mwanakwerekwe/Fuoni imekwenda vizuri na tunaishukuru serikali kwa juhudi yake na tunamshukuru Mhe. Rais wetu kwa juhudi yake, kwa sababu kulikuwa na maneno mengi yanasemwa kwamba ah, hawana uwezo wa kufanya lolote lakini uwezekano wake upo na umeonekana na kila mtu alikuwa anasema haliwi lakini ndio limekuwa.

Je, hivi sasa Mhe. Spika, umefika wakati kuwa na staha zetu katika barabara na katika mji wetu ukitoka Mjini kuelekea Fuoni, Mwera, Bububu mpaka Maungani na kwengineko ni maeneo ambayo yanafaa kuwekwa taa za barabarani, lakini Mwanakwerekwe bado haijakamilika mambo yake kabla kuja kuvunjwa baadae wizara ina mpango gani kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa juu ya kuweka angalau alama za mataa yetu ili pang'are na usalama upatikane barabara hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, sisi tunataka kuhakikisha barabara zote tunaziwekea alama na vile vile taa kwa sababu pia zinapunguza ajali. Sasa pale kadri ya fedha tutapozipata basi hatua tutazichukua kukamilisha na kuondosha tatizo la alama barabarani pamoja na kuweka taa katika barabara hizo kwani pia unapendezesha mji kama hivi sasa mji unavyong'ara na kupendeza katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi.

Nam. 27

Ukosefu wa Huduma za Afya Katika Kituo cha Chaani

(Mheshimiwa Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondosha)

Nam. 30

Ujenzi wa Hospitali ya Mbuzini

Mhe. Machano Othman Said – Aliuliza:-

Moja ya mambo ambayo yanapewa kipaumbele na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuwapatia wananchi wake huduma nzuri za afya na katika kutimiza lengo hilo, serikali imekuwa ikijitahidi kujenga hospitali na vituo vya afya sehemu mbali mbali. Miongoni mwa hospitali hizo ni ya Mbuzini, Wilaya ya Magharibi "A" ambayo imepata bahati ya kutembelewa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zaidi ya mara mbili na katika ziara zake hizo Mhe. Rais, alitaka Wizara ya Afya kufanya haraka ili kumaliza ujenzi wa hospitali hiyo ili iwe hospitali ya Wilaya.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa hospitali hiyo katika kutekekelza agizo la Mhe. Rais na kuwapunguzia usumbufu wa ukosefu wa huduma bora wananchi wa Wilaya ya Magharibi "A".

(b) Ni lini ujenzi wa hospitali hiyo unatarajiwa kuanza tena.

(c) Hivi sasa kuna mazungumzo yoyote baina ya wizara yako na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, ambao ndio waanzilishi wa hospitali hiyo, katika kupanga mpango mkakati wa kumalizia ujenzi wa hospitai hiyo na uendeshaji wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Afya inaendelea na hatua za utekelezaji wa agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kuendeleza ujenzi wa jengo la hospitali ya Mbuzini ambayo azma yake ni kufanywa kua hospitali ya Wilaya. Katika kulitekeleza agizo hilo, wizara imeshafanya mazungumzo na waanzilishi wa ujenzi huo ambao ni kwa sasa hivi ni Manispaa ya Magharibi ”A”. Pia, imeshafanya mazungumzo na wafadhili mbali mbali ili kuweza kusaidia ujenzi huo.

Mhe. Spika, kwa kuanzia, ujenzi wa hospitali hiyo umeingizwa katika mpango wa ujenzi chini ya ufadhili wa *Milele Foundation* ili iweze kutoa huduma za kituo cha daraja la pili kabla ya kupandishwa daraja na kuwa hospitali ya Wilaya kama ilivyoagizwa wakati wa ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuandaa mchoro wa hospitali hiyo, gharama za ujenzi hadi kukamilika kwake.

Mhe. Spika, ujenzi wa hospitali hiyo unatarajiwa kuanza mara baada ya wafadhili *Milele Foundation* kumaliza ujenzi wa vituo vinne vya Pemba na kuendelea na vituo vya Unguja ikiwemo kituo cha Jang’ombe Urusi, Tazari, Mtende, Mpapa, Charawe, Mtoni, Kiyanga na hospitali ya Mbuzini ambayo tutahakikisha inapata kipaumbele kwa umuhimu wake. Ahsante.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika majibu mama ni kwamba endapo maagizo ya Mhe. Rais yamechukua muda mrefu kutekelezwa napenda nifahamishe kwamba maagizo hayo yatatekelezwa lini na lini wakati Wilaya ya Magharibi ”A” ina idadi ya watu ikiwa ya pili kwa Zanzibar.

a) Je, nataka kumuuliza haoni kwamba hata bajeti ya 2017/2018 itakuwa bado kumalizwa kujengwa kwa hospitali hiyo.

b) Kwa kuwa serikali kupitia *Milele Foundation* inataka kujenga vituo vingi, haoni kwamba ni vyema kumalizia kituo cha afya cha Bubwisudi ambacho Mhe. Naibu Waziri, ambaye sasa ni waziri na Katibu Mkuu mstaafu wa wizara hii walijitahidi sana kusimamia

ujenzi wa kituo hicho kupitia *Milele Foundation* haioni kwamba wakimalize ili kuwapunguzia kero wananchi wa Mbuzini, Mkanyageni, Kitundu na Bubwisudi yenyewe wakati wakisubiria kumalizika kwa ujenzi wa hospitali ya Mbuzini

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza namuomba Mhe. Mwakilishi yeye pamoja na wananchi wa jimbo lake muondoe wasi wasi kwamba kutakuwa na ucheleweshaji wowote wa ujenzi wa hospitali hiyo, nimesema mara baada ya kumaliza vituo vya Pemba. Vituo vya Pemba vinne vinamalizika Januari, na Januari hiyo hiyo tunategemea kwa uwezo wa *Allah* mpango wa kuanza vituo vya Unguja utakuwa umeshakamilika. Kwa hiyo, kuhusu ucheleweshwaji wa ujenzi wa hospitali hii ya Mbuzini basi ondoa wasi wasi na sisi wizara tumeshalibeba kwamba tutaipa kipaumbele kuhakikisha kwamba inapewa *first priority* inamalizika kwa haraka.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, vituo vingi vya afya hususan vilivyomo katika jimbo langu la Ziwani kama vile Wesha, Mbuzini na Ziwani kuna upungufu wa madaktari na ma-*orderly*. Je, wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wamepatikana madaktari katika vituo vile ili wananchi kupata huduma kama ipasavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Wizara ya Afya, inahamu sana ya kufanya uajiri kwa sababu kweli tunakiri kwamba tunaupungufu ya *staff* na tumeshapeleka maombi katika wizara inayohusika ya kupatiwa uajiri, naamini na nataka ukubali na utulie kwa suala hili kwamba, wizara inayohusika na uajiri itakapopata tu ruhusa ya kuajiri na uwezo wa kuajiri, basi itaajiri na katika vituo vyako vya Ziwani na vyengine kwenye jimbo lako utapata ma-*orderly* na wafanyakazi waliotajwa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali umekwisha na kabla hatujaendelea nilikuwa nina tangazo moja tu. Waheshimiwa Wajumbe, ambao ni wajumbe wa Kamati ya Uongozi nilikuwa nakuombeni mara baada ya kuahirishwa saa 7:00 mchana tukutane juu katika ukumbi wa mikutano kidogo kwa ajili ya majadiliano na Spika. Baada ya hapo sasa naomba nimwite Katibu kwa shughuli inayoendelea.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, nikushukuru sana Kanuni ya 63, 67 ndio iliyonisimamisha hapa, sijui utaniruhusu nisome au?

Mhe. Spika: Isome wasikie Waheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante.

Mhe. Spika, kuhusu taarifa inakuja kifungu cha 67, ukurasa wa 21, shughuli za kikao za Baraza zitafanywa kwa utaratibu ufuatao kulingana na shughuli zitakazokuwepo katika kikao. Hoja yangu kwenye kifungu (j) maelezo binafsi ya Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, ukurasa wa ngapi?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ukurasa wa 21, Kanuni ya 27, niliyoisoma mimi shughuli za kikao cha Baraza zitafanywa kwa utaratibu ufuatao kulingana na shughuli zitakazokuwepo katika kikao. Hoja yangu ipo kwenye kifungu (j) maelezo binafsi ya mjumbe.

Mhe. Spika: Naam! Tupe hayo maelezo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii Kanuni ya 27(j) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, nichukue fursa hii kutanguliza shukurani zangu kwa uwezo wake wa kutupa uhai na uzima mpaka dakika hii, nakushukuru na wewe kuniruhusu kwa dakika chache kuwasilisha maelezo yangu binafsi kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Baraza.

Mhe. Spika, hoja yangu hapa kubwa katika uzinduzi uliofanyika juzi Jumamosi huko Mkoani Pemba.

Mhe. Spika, nia na madhumuni ya maelezo haya ni kutambua, kuthamini na kupongeza kwa dhati juhudi za kazi kubwa inayofanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein katika kipindi kifupi cha awamu zake za uongozi ameleta mambo makubwa ambayo mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Paje, natumia fursa hii kikanuni kumpongeza kwa dhati kutoka ndani ya sakafu ya moyo wangu.

Mhe. Spika, Waswahili wanasema 'mtu haki yake apewe au mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni' kwa kusema Dkt. Ali Mohammed Shein apewe haki yake katika kipindi cha uongozi wake hasa katika sekta ya afya. Usafirishaji tumeshuhudia amenunua meli kwa gharama kubwa na meli ya kileo, miundombinu hatua kubwa na hivi sasa ndege Pemba zinatua usiku. Pia, nitumie *Suratul Dhuha* aya ya 11, inayosema "*waama binii'mati rabika fahadith*" maana yake nini Waheshimiwa Wajumbe? Na neema ya Mola wako isimulie kwa kushukuru au kwa kufanya matendo mema. Kwa hiyo, tumshukuru Dkt. Shein.

Mhe. Spika, Dkt. Ali Mohammed Shein, amefanya kazi kubwa katika kufanikisha ujenzi mpya wa hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani ambayo imejengwa upya na ndugu zetu wa kufaana na sio wa kufanana wa Jamhuri ya Watu wa China, nao nawapongeza sana. Mhe. Spika, ujenzi umefanywa mambo makubwa katika jengo lile kuna sehemu ya utawala, jengo la huduma za dharura, jengo la huduma la uchunguzi na upasuaji, jengo la huduma ya wazazi, wodi ya wanawake, jiko la kupikia, sehemu ya kufulia, ghala ya madawa, sehemu ya kuchomea taka na kuhifadhia.

Mhe. Spika, kama hapo hapatoshi kuna huduma ya *CT-Scan*, kuna mashine tatu za *X-Ray* mpya, vyumba vinne vya upasuaji, *ultrasound.* Mheshimiwa, tusipoteze muda kuna mengi, kuimarisha huduma za mama wajawazito na kuondoa malipo ya huduma hapo, kuimarisha huduma za *ICU* za kisasa. Nampongeza sana Mhe. Rais, kwamba mwezi haujafika tangu amefungua jengo jipya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, niendelee katika Sekta ya Usafirishaji (anga), kazi kubwa wamefanya na kuimarisha Uwanja wa Ndege Pemba na kuweka taa na maendeleo ya ujenzi wa jengo jipya la abiria unaendelea.

Mhe.Spika, katika Sekta ya Usafiri Baharini Dkt. Ali Mohammed Shein amefanikisha kutafuta usafiri wa uhakika baina ya visiwa vya Unguja na Pemba na Dar-es-Salaam kwa kununua meli mpya yenye uwezo wa kuchukua abiria wengi na mizigo, nimpongeze kwa hilo.

Mheshimiwa, yako mengi na hivi sasa nasikia kuna harufu tu, huenda Hospitali ya *Mental* nayo ikafanyiwa marekebisho makubwa na Hospitali ya Wazazi, Mwembeladu. Imani yangu kwa Dkt. Ali Mohammed Shein ataendelea na juhudi zake za mipango kwa kuwatumikia Wazanzibari na namuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu na afya njema aendelee na ari ya kutekeleza

ahadi zake na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo kama inavyosema sasa.

Mhe. Spika, namalizia maelezo yangu mafupi kwa kusema kwamba, ni wajibu wetu Wawakilishi kupongeza na kutambua yale yote mazuri yanayofanywa na viongozi wetu. Wananchi wanaona, lakini na sisi tuna wajibu wa kupongeza kwa kuwapa moyo na kuwatia ari zaidi.

Aidha, ni wajibu wetu pia kuelekeza, kukosoa na kutoa ushauri pale tunapoona mambo mazuri yanayofanywa na viongozi wetu yanatia dosari, baadhi ya watendaji wasiotaka kushauriwa wala kufuata taratibu zilizowekwa na nchi katika kutekeleza majukumu yao, kwa kujua au kutokujua na kwa kufanya wajibu wetu na sisi Wajumbe wa Baraza hatutafuti umaarufu wala sifa na kujionesha, kwani hayo tunayoyafanya ni majukumu yetu kikatiba. Mhe. Spika, sitafuti umaarufu wala kujionesha.

Mhe. Spika, kwa kumalizia baada ya kueleza hayo nakushukuru kwa kunipa fursa hii kwa kusema maelezo yangu binafsi na nimpongeze Dkt. Ali Mohammed Shein pamoja na wasaidizi wake, Mzee wetu Balozi Seif Ali Iddi kwa hekima na busara zake ambazo zimetusaidia katika kufanikisha maendeleo hayo.

Mhe. Spika, niweke sawa, hivi juzi Alhamisi nilileta hoja ya umeme, lakini baada ya kukaa na washauri au wenzangu kunambia kuna pahali Jaku Hashim umeteleza na mimi ni binaadamu, hakuna mkamilifu isipokuwa mmoja, Ulimi hauna mfupa na hapa hata Mhe. Haji Omar Kheir, kuna siku alimuomba radhi Dkt. Mwinyihaji Makame, ndio binaadamu. Nilisema, haya ndio maamuzi ya Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri, tumekutana na Mhe. Rais, niombe kwa kusema kuondosha usemi ule, ninachosema nikuombeni radhi kwa maamuzi niliyoyapitisha kule, nilichosema haya ndio maamuzi ya Baraza la Mapinduzi. Kwa hiyo, nataka kuweka *Hansard* sawa kwa kufuta usemi ule, nikuombe radhi kama kuna kosa nimefanya sio kwa nia ya makusudi, unajua ukishakaa kwenye chombo hiki, ulimi hauna mfupa.

Mhe. Spika, naomba niseme hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, umefanya mambo mawili, kwanza umetambua mchango mkubwa ambao Mhe. Rais, anaufanya kwenye nchi na kutambua pia mashirikiano ambayo Mhe. Rais, anayapata

kutoka kwa wale ambao amewateuwa ni jambo zuri. Lakini pia napenda nikupongeze kwa hili la kujaribu kuweka sawa lugha yako uliyoitumia kwa kuomba radhi. Huo ndio uungwana, sote ni wanaadamu inapotokezea mambo kama haya mtu amekosea katika kauli zake basi ni vyema sana aombe radhi na sisi tuseme kwamba *Hansard* irekebishe ili yale maneno yasiwe kama vile ambavyo yalikuwa au yamejitokeza, iwe kwamba kusudio lako lilikuwa vyengine. Nashukuru sana.

Katibu kwa shughuli inayoendelea, tafadhali.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya 2016

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita Mhe. Waziri, naomba nimpishe Mhe. Mwenyekiti ili aje aendelee na Baraza, tafadhali.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya na uzima na kutuwezesha kukutana tena leo hii katika Baraza hili la kutunga sheria, kuendeleza kazi zetu kwa amani na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wewe, Mhe. Spika, na Mhe. Naibu Spika, kwa juhudi zenu na jitihada thabiti za kufanikisha mswada huu kuwezesha kuwasilishwa katika kikao hiki kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa aina ya kipekee naomba kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni pamoja na Makamo wake Mhe. Hamida Abdalla Issa, Viti Maalum na Wajumbe wote wa kamati hii kwa mashirikiano yao na kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuupitia mswada huu na kupendekeza marekebisho ya kuzingatiwa. Juhudi na michango yao tunaithamini sana na tunaipokea.

Aidha, nawashukuru sana Makatibu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuisaidia kamati kukamilisha kazi yao muhimu ya kuupitia Mswada wa Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kutoa shukurani kwa kumshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wanasheria wa ofisi yake kwa kusaidia kuandaa Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2005 na kwa kufanya tafsiri ya Kiswahili kwa umahiri mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Ndugu Khamis Mussa Omar; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ali Khamis na Mkurugenzi Mipango, Sera na Uendeshaji, Saumu Dau na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na uongozi na wafanyakazi wote wa *ZSSF* kwa kazi kubwa ya kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kufanikisha uandaaji wa Mswada wa Sheria hii.

Nawashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao yote waliyoitoa katika semina ya kujenga uelewa wa mswada huu iliyofanyika jana. Maoni na michango yao tumeisikia na tutaizingatia katika hatua mbali mbali za utekelezaji wa sheria hii mara baada ya Waheshimiwa kuipitisha na kuwekwa saini na Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Nam. 2 ya Mwaka 2005, yanalenga kuufanya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii uwe imara na endelevu kwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza baada ya matokeo ya tathmini zilizofanyika.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ulianzishwa rasmi kwa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar Nam. 2 ya Mwaka 1998. Sheria hii ilikuwa na madhumuni ya kuanzisha taasisi ya kusimamia masuala ya hifadhi ya jamii na kuweka utaratibu bora wa hifadhi ya jamii kwa wafanyakazi wa sekta rasmi wanapofikia umri wa kustaafu. Sheria hii ilifanyiwa marekebisho ya kwanza mwaka 2000 kwa lengo la kuweka mazingira bora zaidi ya kuuwezesha Mfuko kuendeshwa kwa ufanisi na kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2005 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Ulimwenguni (*ILO*), ilizifanyia mapitio sheria zote za kazi na kubaini upungufu uliopelekea kuundwa kwa Sheria Nam.2 ya Mwaka 2005 kwa madhumuni yale yale ya kuweka mazingira mazuri ya mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho yaliyofanywa mwaka 2005 yalilenga zaidi katika maeneo yafuatayo:

1. Kuweka usawa wa umri wa kustaafu baina ya wanawake na kwa wakati huo ilikuwa miaka 50,wanaume wao walikuwa miaka 55 na kuwa miaka 60 kwa lazima na 55 kwa hiari kwa jinsia zote, na

2. Kutumia wastani wa miezi 60 badala ya mshahara wa mwisho katika kukokotoa malipo ya mafao kwa wastaafu.

Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyo utaratibu wa kawaida, Mfuko umekuwa ukifanyiwa tathmini maana ya *Curio Evaluation* katika vipindi tofauti, kwa lengo la kuangalia uwezo wa kifedha katika kutekeleza majukumu yake. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umefanyiwa tathmini na Shirika la Kazi Ulimwenguni (*ILO*) mwaka 2006, Kampuni ya *Cadogan Financial Service* nayo ilifanya tathmini mwaka 2010, lakini vile vile Kampuni ya *Muhanna & Tour Acura Service* nayo ilifanya tathmini mwaka 2011.Tathmini ya mwisho ni ya mwaka 2015 ambayo ilijumuisha Idara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi matokeo ya tathmini zote hizo yanabainisha kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar utakabiliana na hali tatanishi katika miaka ijayo kutokana na mfumo wa uendeshaji wake. Miongoni mwa sababu zilizoainishwa ambazo zinachangia hali ya Mfuko kutokuwa endelevu ni hizi zifuatazo:-

1. Viwango vidogo vya uchangiaji, kwa maana ya asilimia 15 ya mshahara ikilingnishwa na asilimia 20 inayochangiwa na Mifuko mingine iliyopo ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

2. Ukubwa wa mafao (kiinua mgongo) yanayolipwa na Mfuko ambayo ni asilimia 300 ya mchango wa mchangiaji ikilinganishwa na ulipaji wa mafao katika Mifuko mingine ambapo ilipwaji wa mafao hayo hauzidi asilimia mia moja.

3. Muda mdogo unaostahili kulipwa mafao kwa mchangiaji, ambao kwa sasa ni miaka mitano ikilinganishwa na miaka 15 inayotumika katika Mifuko mingine ya ukanda wa Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia kasoro zilizopo imeonekana kuna haja ya kurekebisha baadhi ya vifungu vilivyomo katika Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya Mwaka 2005 ili kuwezesha Mfuko kuwa endelevu katika uendeshaji wa shughuli zake.

Mhe.Mwenyekiti,miongoni mwa mapendekezo yanayokusudiwa kufanywa ni kama ifuatavyo:-

1. Kuongeza viwango vya kuchangia kwa watumishi kutoka asilimia 15 hadi asilimia 20 kwa uiyano wa asilimia 13 kutoka kwa muajiri na asilimia saba kutoka kwa muajiriwa.

2. Kuongeza muda wa kuchangia ili kustahiki kupata mafao ya uzeeni kutoka miaka mitano ya sasa hadi miaka 13.

3. Kubadilisha namna ya ukokotoaji wa mafao katika Jadweli la Kwanza kifungu cha 1(1)(a), (b), (c) na kifungu cha 1(2) chenye vipengele (a), (b), (c) kinachoonesha mgawanyo wa michango kwa mafao yatakayolipwa na kifungu cha 1(3), kipengele (a) na (b) kinachoonesha mgawanyo wa kiwango cha michango inayolipwa baina ya muajiri na muajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, kupitishwa marekebisho ya sheria hii kutaleta faida nyingi sana ikiwemo kuongeza wigo wa wanachama kwa kuingiza makundi mengine katika sheria, ikiwemo sekta isiyo rasmi. Wananchi waliojiajiri wenyewe, Wazanzibari wanaishi nje ya nchi (Diaspora) na wastaafu. Aidha, faida nyengine zitakazopatikana ni kuongezeka kwa pencheni kwa wastaafu kwa asilimia 25 na pili kuwa na sheria itakayohakikisha Mfuko unakuwa endelevu na tatu kuanzisha kiwango cha chini na cha juu (ukomo) cha malipo ya pencheni ya mwezi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Hamida Abdalla Issa (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya Mwaka 2005, Kuweka Masharti Bora zaidi kwa ajili ya Ufanisi na Usimamizi imara wa Mfuko na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naanza kusoma hotuba hii kwa kutaja jina la Mola Mtukufu, aliyeiwezesha Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo kuupitia na hatimaye kuurekebisha Mswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya

2005, na kuniwezesha kusimama leo hii mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha maoni ya kamati hii kuhusu mswada huo.

Kamati yetu inatoa shukurani za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kumteuwa aliyekuwa Mjumbe wetu Mhe. Shadya Mohammed Suleiman. kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto. Sambamba na hayo, kamati inampongeza sana Mhe. Naibu Waziri mteule Mhe. Shadya Mohammed, kwa uteuzi huo. Tunaamini kuwa, kuteuliwa kwake ni ishara ya utendaji wake bora kwenye nafasi mbali mbali alizowahi kushika.Tunamtakia kila la kheri na utekelezaji mwema wa majukumu hayo mapya ya Kitaifa. Aidha, tunawapongeza Manaibu Waziri wapya Mhe. Mihayo Juma N'hunga na Mhe. Shamata Shaame Khamis, kwa kuteuliwa kwao kwa nafasi hizo, tunawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yao kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, tunaupongeza uongozi mzima wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, wakiwemo Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dr. Khalid Salum, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Ndugu Khamis Mussa pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa *ZSSF* Ndugu Abdulwakil kwa kuamuwa kuja na marekebisho ya sheria hii kwa lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za Mfuko kwa maslahi ya wanachama wake. Madhumuni makuu ya kufanya marekebisho hayo ni kuimarisha mfumo wa kisheria kwa kuyaondoa mapungufu yaliyojitokeza katika sheria ya awali na kuweka masharti mapya kwa nia ya kutoa huduma bora kwa wanachama wake. Marekebisho haya pamoja na mambo mengine, yatatoa fursa kwa baadhi ya wanachama kuweza kujiunga katika Mfuko wakiwemo wanachama kutoka sekta zisizo rasmi, wanachama waliojiajiri wenyewe, Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi pamoja na makundi maalum. Vile vile, marekebisho haya yamejikita katika kuangalia upya utaratibu mzuri wa ukokotoaji wa pencheni, mafao na viinua mgongo kwa wanachama wa Mfuko.

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilikutana na Wizara ya Fedha na Mipango tarehe 18/11/2016 na kuupitia mswada wa *ZSSF* kifungu kwa kifungu, wakati kamati yangu inaupitia Mswada huu, ilifanya baadhi ya marekebisho ya msingi kwa lengo la kuboresha Mswada huu. Baadhi ya marekebisho hayo naomba niyaeleze katika hotuba hii na mengine yataonekana katika nakala ya Marekebisho ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi Mswada huu umependekeza marekebisho ya michango ya wanachama kutoka asilimia 15 hadi 20 ambayo yatawagusa wanachama wa Mfuko na waajiri wao kama ilivyoelezwa kwenye Jadweli la kwanza la Sheria hii. Kwa mnasaba wa mabadiliko hayo, mwanachama atachangia katika Mfuko asilimia 7 ya mshahara wake wa mwezi na mwajiri atawajibika kuchangia asilimia 13 ya jumla ya mshahara wa mwezi anaolipwa mwanachama. Mabadiliko haya ni mazuri kwa upande mmoja kwani yataongeza uwezo wa Mfuko kuwa na makusanyo makubwa na kuweza kutoa huduma mbali mbali kwa wanachama wake kwa nia ya kuendeleza na kuimarisha Mfuko huo.

Kwa upande wa ongezeko la mchango wa mwajiri kutoka asilimia 10 hadi 13 ina umuhimu wake, lakini pia kamati yangu inapenda kutoa angalizo kuwa ongezeko hili linaweza kuleta athari za kiuchumi kwani linaweza kupunguza uwezo wa kutoa ajira kwa vijana wetu katika sekta binafsi. Kiuhalisia, ongezeko hili la uchangiaji kwa muwajiri litawasukuma waajiri wa sekta binafsi nchini kuongeza bei za bidhaa na huduma zao jambo ambalo linaweza kuifanya Zanzibar kutomudu ushindani wa biashara ya Kimataifa kwa kuzalisha kwa gharama kubwa na uuzaji wa bidhaa zenye bei kubwa na hivyo kuiweka nchi yetu kwenye hali mbaya kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Ukokotoaji wa pencheni kwa kigezo cha asilimia 36 ya wastani wa mwisho wa mshahara ambao umeelezwa kwenye Jadweli la kwanza utaongeza mzigo mkubwa wa malipo kwa wanachama wa Mfuko kila inapotokea nyongeza ya mshahara kiasi cha kutishia uhai wa Mfuko.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba niende moja kwa moja katika baadhi ya vifungu ambavyo tulivifanyia marekebisho, kama hivi ifuatavyo:

Kifungu cha 17(4)(a) cha sheria mama kinaeleza kosa la kutochangia kikamilifu kwa wanachama wa Mfuko na kutoa adhabu ya faini isiyopungua shilingi Milioni Tano za Kitanzania au kifungo cha mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja faini na kifungo.

Pamoja na kuwepo adhabu hizi kwa mujibu wa Sheria lakini bado Kamati inapendekeza hatua muwafaka zichukuliwe kwanza kabla ya kumfikisha aliyetenda kosa Mahkamani kwa lengo la kujenga mahusiano mazuri baina ya mwanacha au Muwajiri na Mfuko. Hali hii itawafanya wanachama na Waajiri kuwa rafiki na Mfuko na kupelekea Mfuko kupata wachangiaji wengi zaidi wa hiari katika kufikia malengo ya Mfuko na hifadhi ya jamii kwa wote.

Mhe. Mwenyekiti Kifungu cha 7(3) cha Mswada huu kinaeleza kama ifuatavyo:

"Waziri ana uwezo wa kuchelewesha mafao ya aina yoyote kutokana na sababu ambazo atajiridhisha kwamba mfuko hauna uwezo wa kulipa mafao hayo kwa wakati huo kwa mujibu wa masharti ya sheria hii".

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilifanya marekebisho katika kifungu hiki kuongezwa maneno "kwa kushirikiana na bodi" baina ya neno "Waziri" na "anao" ili kutoa fursa nzuri zaidi kwa bodi ya *ZSSF* kushiriki katika maamuzi yanayohusu ustawi wa Mfuko na wanachama wake.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, Kamati yangu ilifanya marekebisho katika kifungu cha 5 cha Mswada ambacho kinarekebisha kifungu cha 17(3) cha Sheria mama. Kifungu kilichopendekezwa katika Mswada kimeweka sharti la uwasilishaji wa michango kwa mwanachama wa Mfuko lakini hakikuonesha dhima ya uwasilishaji wa mchango kwa muajiri. Kwa mnasaba huo, Kamati yangu ilifanya marekebisho katika kifungu hiki kwa kuweka dhima ya muajiri katika kuwasilisha michango ya wanachama kwa Mfuko. Kwahivyo, kifungu hiki baada ya marekebisho kitasomeka kama ifuatavyo:

"Mchango wa mwanachama na muajiri chini ya kifungu hiki, utawasilishwa na muajiri katika Mfuko kwa utaratibu utakaowekwa ndani ya siku kumi na tano baada ya mwisho wa mwezi husika"

Mhe. Mwenyekiti, pia, Kamati yangu ilifanya marekebisho katika kifungu cha 13 cha Mswada ambacho kinarekebisha kifungu cha 44(3) cha Sheria mama kwa kuingiza marekebisho mapya ya kifungu cha 44(3) cha Sheria mama. Kifungu hiki kabla ya marekebisho kilikuwa kinatoa mamlaka kwa Waziri baada ya kushauriana na Boadi, kurekebisha masharti ya vifungu vya jadweli la kwanza la Sheria hii. Lakini kwakuwa Sheria hii ina jumla ya majadweli matatu (3) Kamati iliona kuwa ni bora mamlaka ya Waziri kurekebisha majadweli isiwe tu katika jadweli la kwanza na badala yake iwe ni katika majadweli yote yaliyopo chini ya Sheria hii. Kwahivyo, baada ya marekebisho hayo, kifungu hiki sasa kitasomeka kama ifuatavyo;

> **"**Waziri kwa kushauriana na Bodi, anaweza kurekebisha jadweli zilizo chini ya Sheria hii"

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waujadili kwa kina Mswada huu na hatimae kuupitisha

kwa lengo la kuuboresha kwa ajili ya kuimarisha huduma za Mfuko. Pia, Kamati yangu inawashauri Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kujiunga katika Mfuko huu kwa lengo la kujiwekea akiba ya uzeeni na kuimarisha Mfuko wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa umahiri na umakini wao waliouonyesha wakati wote wa kutekeleza jukumu hili la msingi la kupitia mswada huu.

Mwisho kabisa, shukrani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mashirikiano makubwa waliotoa kwa Wizara kwa lengo la kufanikisha jukumu hili la msingi. Naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Mjumbe
4.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Mjumbe
5.	Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Mjumbe
6.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Mjumbe
7.	Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
8.	Ndg. Salum Kamis Rashid	-	Katibu
9.	Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, nachukuwa fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na usikivu wa hali ya juu waliouonesha wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Makamu Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti, kwa uwasilishaji wako.

Waheshimiwa Wajumbe katika meza yangu hapa nina mchangiaji ambaye ni mmoja tu hadi hivi sasa inaelekea kwamba mmeridhika katika semina ya jana hamna maswali tena. Kwa hivyo, sasa ni zamu ya kuchangia na sasa namwita mchangiaji Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata).

Mhe. Ali Suleiman Ali (**Shihata**): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa mbele

ya Baraza lako tukufu kuchangia mswada huu kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii namba 2 ya mwaka 2005.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote na wataalamu mbali mbali waliona pana haja kwa sasa hivi kupata mfuko huu na kuuchangia au kufanya marekebisho kwa maslahi ya wanachama wa mfuko huu.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni sehemu muhimu kwa wananchi wetu hasa wafanyakazi katika serikali kama nilivyosema katika sekta binafsi na kwa sasa hivi unavyotaka kuweka itakuwa vizuri, kwamba wajasiriamali mbali mbali wanaweza kujiunga katika mfuko huu wakitimiza masharti yanayotakiwa ili kujinasua katika maisha yao ya baadae. Dhamira ya Serikali Mhe. Mwenyekiti, kuhakikisha kwamba mfanyakazi anafanya kazi kwenye mazingira yanayokubalika kidunia au kimataifa, kwa sababu mashirika haya ndio huwa kama benki yao ya baadae huko mbele katika maisha ya uzeeni au baada ya kustaafu.

Kwa hivyo, mimi niipongeze serikali na nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuona kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni kioo na kwa Zanzibar ni sehemu ambayo tunaitegemea kwa wananchi wetu ambao ni wafanyakazi wa serikali hata sekta binafsi itawagusa.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko tunautegemea kwa mambo mengi hasa tukizingatia kwamba faida yake huwa ni kubwa kwa mfanyakazi lakini na mfuko unatakiwa vile vile utafute mbinu za kupata fedha ili kujiweka vizuri zaidi kwa huduma zake kwa wananchi au kwa wafanyakazi ambao inawategemea iwalipe au mambo mengine ambayo anakubaliana nayo.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, mfuko madhumuni yake mengi sana lakini mengine ambayo yanagusa katika moja ambalo nimelipenda sana katika maisha ya mfuko huu kuna mgawanyo ambao unakubalika wameufanya utaratibu mzuri kwa walengwa wa mfuko huo yaani "mafao". Kuona mafao ya uzeeni, urithi na ulemavu mfuko huo asilimia 17 ili kusaidia katika shughuli yao hiyo au katika mambo hayo yanayojitokeza.

Lakini pia mafao ya uzazi kuna asilimia 1 kuna utaratibu mzuri wameupanga hapa nao unanufaisha. Lakini mfuko pia una mafao ya matibabu una asilimia 2. Hii yote ni kuwajali wafanyakazi wake na kuhakikisha kwamba huu ni kama ni wanachama au mwanachama anahusika kupata mambo mbali mbali katika kujiendesha katika mambo maisha hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mfuko huu uliponzishwa ulikuwa na mambo mengi na kulikuwa na maneno mengi. Maneno makubwa ambayo yalikuwa yanajitokeza kuna wafanyakazi ambao wengine wako serikalini, wengine wako katika sekta binafsi na kwa Zanzibar tunachukulia kwamba sekta binafsi imechukua asilimia kubwa ya uajiri katika wananchi wetu ambao mfuko huu pia unawaingiza na lazima uwaingize kutokana na sheria za mfuko. Lakini shida inayojitokeza hapo baadae wafanyakazi katika sekta binafsi hasa katika mahoteli mara nyingi huwa wanakatishwa au wanaachishwa kazi huwa na manung'uniko makubwa yanajitokeza.

Mimi ombi langu ili twende vizuri mwanachama ni mtu anayetaka kuelimishwa, na mfuko ili uendelee vizuri uwe na darasa tosha la kuelimsiha wanachama wake kuondoa migogoro mbali mbali na kuweka ufanisi katika kazi zao na kuhakikisha kwamba mwanachama atakuwa anajielewa, mimi kadiri ya kuchangia kwangu nina miaka yangu mitano mfano lakini linapotokea tatizo jengine kuna hili, lakini kuna kustaafu kwa hiari au kustaafu kwa lazima kwa haya yote ningemuomba sana Mhe. Waziri akayaangalia ili somo la darasa katika mfuko huu kuwaelimisha wanachama wake ni jambo muhimu kuliko mengineyo.

Ili kumuelimisha mwananchi ataelewa huyu mfanyakazi na ikiwa hukumuelimisha kujiunga kwake pia ni hatari kwa sababu atakuwa anaona kuwa mimi nimefanya kazi nimeacha hoteli au nimeachishwa au nimefukuzwa pia inatokea. Kwa hivyo, watu hawa wawekewe vidodoso maalumu katika kujiunga tu katika mfuko huu basi pawe na taarifa moja, mbili, tatu aipate yule mwanachama ili aelewe sharti langu la kwanza liko moja, la pili, la tatu mpaka kufikia mwisho itakuwa manung'uniko ya hapa na pale yataondoka Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii mimi nimshukuru Mkurugenzi wake na watendaji wake wote kwa muda huu ambao tuko nae au tuko nao mambo mengi yamejitokeza mafanikio katika nchi yetu, kuna majengo mazuri ya kileo yamejengwa, kuna viwanja vyetu vya watoto tumeviona, kuna mambo mengine mengi, mnara wetu wa Michenzani tumeuona kutimia miaka 50 ile ni historia ya nchi yetu. Lakini na mengi wanafanya.

Sasa mimi natoa rai au naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kujenga nyumba ni sehemu moja ya mradi wetu huu au ya mfuko wetu huu, lakini unapomkodisha mfanyakazi unaweza kupata chochote. Lakini kuna mwananchi wa kawaida hafaidiki sana hana uwezo siku nyengine kukodi sehemu ile au kukodi nyumba zile.

Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kupitia Wizara ya Fedha tubadilike, tuelekee katika muelekeo wa kujitajirisha haraka haraka si kwa kunyang'anya lakini mfuko nataka uongeze mapato yake kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, dunia ya leo ni biashara na mfuko huu unaendeshwa kibiashara, mimi ningeomba tu tutafute maeneo ya Unguja na Pemba tuweke viwanda vyetu; kuna viwanda mbali mbali tunapiga kelele nchi yetu. Mimi napiga kelele kila nikisimama hapa kuna viwanda masikini vilikuwa viwanda vya samaki, viwanda vya mwani, viwanda vya tungule, ambapo tungule sasa hivi kwa Zanzibar tunasema kwamba wenzetu hivi sasa wananchi wameamka Bara wanapiga kelele kwamba tungule zao hazitakiwi Unguja na naweza kusema kwamba kwa asilimia kubwa tuwapongeze wakulima wetu wa Zanzibar, hivi sasa hivi wameamka vizuri na wako vizuri katika kuongeza kasi ya maendeleo katika uboreshaji wa kuleta maendeleo ya ulimaji wa mboga mboga.

Kwa hivyo, hii ni moja itatusaidia kama patakuwa na viwanda vya kushindika mazao yao haya yatawasaidia. Lakini pia kuna msimu Mhe. Mwenyekiti, kuna msimu wa mananasi. Mananasi yanatokea wakati mwengine vya kuyafanya huna. Kwa hivyo, pia tungepata viwanda vyake tukaweza kuviendesha ili mfuko ukajiendeleza zaidi.

Mimi nasema chochote kinaweza kuingia ubia kwa kuwa mfuko una rasilimali fedha, lakini wakatafutwa watu ambao wanaweza kuendesha viwanda hivi kwa faida ya pamoja pia si mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunasema tu kwamba kuna wawezekaji wengi hapa Tanzania lakini kuna mwekezaji wetu mmoja mzalendo wa hapa hapa Said Bakhressa si vibaya kumtaja tunamshukuru anajitahidi katika kuleta ajira katika sehemu zetu mbali mbali na mimi niseme tu kwamba mfuko huu kama utazaa viwanda mbali mbali vijana wetu wengi wa mitaani watapata ajira.

Mhe. Mwenyekiti, ndugu yetu Said Bakhressa ana vibaskeli vinafika elfu ngapi wanaotembeza *Ice Cream*, sasa ile ni ajira na wanaridhika na sehemu kama ile. Kwa hivyo, na sisi si vibaya kuiga, kwa sababu mimi katika maisha yangu nimesema tu kama kuna mwenzangu kalifanya zuri na mimi nataka nimuige yeye nilifanye zuri au zaidi si vibaya maana kuiga mazuri si vibaya, kuiga ubaya ni vibaya lakini kuiba wema si vibaya.

Kwa hivyo, niseme tu Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri tusome kwa wenzetu Mhe. John Pombe Magufuli nakumbuka katika ziara zake za

kufungua majengo makubwa ya *NSSF* Bara nilimshuhudia akasherehekea katika ufunguzi lakini baadae akabadilisha kibao akasema ah mfumo huu sasa hivi haufai tuelekee kwenye viwanda na sasa hivi kwa taarifa tu Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba mifuko miwili ya Hifadhi ya Tanzania Bara kuna *NSSF* na kuna mengine ambayo ipo wamejiandaa kutafuta viwanda katika sehemu mbali mbali, nakiri kwamba Zanzibar tuna bahati mbaya hatuna maeneo ya kutosha. Lakini haya haya finyu tuliyonayo kama tutayadhibiti na tukafanya vizuri basi mfuko huu Mhe. Mwenyekiti utakuwa kwa muda mfupi yaani umekuwa vizuri utaongeza pato lake mara mbili zaidi katika kuwaendeleza wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo namuomba sana Mhe. Waziri tutafute wataalamu mbali mbali kwa sababu mimi nina rasilimali fedha, kwa mfano lakini si uwezo wa kutafuta rasilimali viwanda, tuwatafute wataalamu ambao serikali yetu kupitia mfuko huu hakutokuwa na hasara kutakuwa na faida basi tuingie katika ubia wowote angalau tutawapatia vijana wetu wengi ajira kwa sababu kilio kikubwa Mhe. Mwenyekiti, katika nchi yetu ni ajira.

Lakini nakiri kwamba ajira sio lazima serikalini, ajira kujiajiri wewe mwenyewe na ndio maana sasa hivi nasema tu kwamba vijana wetu wengi kwenye mashamba ya matikiti yameenea sasa hivi, zao la matikiti limeenea halitoki Bara sasa, tungule hazitoki Bara sijui mabilingani nimeshuhudia kwa macho yangu Mhe. Mwenyekiti, yanatoka Unguja yanapelekwa Pemba, sasa hivi hapo nyumba kidogo kwa sababu kila zao linapishana, Pemba zinakuja ndizi huku na cha huku kikenda kule na mabungo yanatoka Pemba lakini na huku yanatoka mabilingani kwa faida ya kule.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nikuombe sana hili suala tuliangalieni kwa kuwa tuna Mhe. Waziri wa Biashara na yeye ndio fani yake katika shughuli zake, wataalamu mbali mbali wanao tufanye kwa bidii yetu yote kuongeza bidii mfuko huu ili kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache kwa kuwa mfuko huu umeboreshwa, lakini ningeomba sana kauli yangu niliopitia kati kati kwamba taaluma ni jambo muhimu kuliko yote, taaluma itawaweka vijana wetu na wanachama wa mfuko huu kuwa na imani, na kwanza ukishajifahamu umejisajili moja, mbili, tatu masharti umeyaelewa huna shida ya kudai mafao pindi linapotokea tatizo.

Kwa hiyo, baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, niseme mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kijito Upele mswada huu

nimeupokea kwa asilimia mia moja na naupitisha, na naomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tutafute rai ya kuuchangia mfuko huu kwa kuisaidia serikali yetu na mfuko huu kwa maslahi ya wafanyakazi wetu. Tunaokerwa mitaani ni sisi Wawakilishi wa Majimbo na wa kuteuliwa na viti maalumu, ukienda huku kuna dosari imetokea utakamatwa Mheshimiwa tusaidie huku, lakini elimu hii na kwa mfumo huu ulioleta Mswada huu sasa hivi naamini elimu ikitoka utakuwa hauna shida wala manung'uniko hakuna. Baada ya hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambao upo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kutoa shukurani na kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kuweza kwa umahiri wao kuwasilisha Mswada huu wa Sheria inayohusiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Vile vile nichukue fursa hii ya kuwepongeza au kuupongeza uongozi mzima wa *ZSSF* kwa juhudi yao hadi kukamilisha kwa taratibu hadi kufika kwa Mswada huu mbele yetu.

Nichukue fursa hii vile vile kuipongeza Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi kubwa sana waliyoifanya usiku na mchana mpaka kuhakikisha kwamba Mswada huu leo unakuja kwenye Baraza. Vile vile nimpongeze msemaji aliyetangulia Mhe. Ali Suleiman Ali na yeye kwa kuuchangia Mswada ulio mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tulifaidika sana jana katika semina waliyotuandalia wenzetu kuhusiana na uelewa wa Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii. Nishukuru sana na nipongeze sana kwa kuratibiwa kwa semina ile. Ilikuwa sina lazima sana ya kuchangia Mswada huu leo kutokana na michango niliyoitoa katika semina ya jana, lakini kwa sababu Baraza hili linasikika na wananchi, ninafikiri hapa ni pahala sahihi pa kuweza vile vile kutoa michango yangu, maswali na pengine nasaha katika kuona kwamba Mswada huu unakwenda vizuri na wafanyakazi na waajiri wananufaika na marekebisho yaliyofanywa katika Sheria hii.

Vile vile kwa sababu nina hofu sana ya Wajumbe pengine usichangiwe na watu wengi, na mimi nikaona nichukue fursa hii vile vile kuweza kuuchangia Mswada huu. Hususan kwa kuzingatia kwamba sisi ni Wawakilishi wa wananchi wanatusikiliza na miongoni mwa kazi zetu ni kuweza kushauri, kuiuliza na vile vile kuwatetea wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa wananchi ni wafanyakazi walioajiriwa na Serikali lakini vile vile walioajiriwa au wanaojiajiri wenyewe kwenye sekta binafsi. Nichukue fursa hii na mimi kuweza kusema machache katika kuuchangia Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaelewa, na baadhi ya Wajumbe wenzetu wanaelewa kutokana na semina ya jana. Wanaelewa juu ya madhumuni, juu ya umuhimu na sababu za marekebisho mbali mbali yaliyofanywa katika kuona kwamba Mfuko wetu wa Hifadhi ya Jamii unaenda vizuri.

Wenzetu wamewasilisha matokeo ya utafiti na wakatwambia kwamba Mfuko wetu wa Hifadhi unaweza ukawa na hali tata, na Mhe. Waziri amekiri katika hotuba yake, ifikapo mwaka 2039 inawezekana kwamba Mfuko ukashindwa kujiendesha iwapo tutaendelea na utaratibu wa michango, viinua mgongo na pencheni ambao unaendelea hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaelewa na hii ni hatari. Na miongoni mwa changamoto iliyosemwa kwamba Mfuko utahitaji msaada wa fedha kutoka Serikalini ili kuweza kulipa mafao na kujiendesha iwapo tutaendelea na viwango hivi vya michango pamoja na mafao mengine ikiwemo pencheni. Hii ni hatari Mhe. Mwenyekiti, na nina imani sisi Wajumbe wa Baraza na wananchi hawatokuwa tayari kuona kwamba Mfuko huu wa Hifadhi itakapofika mwaka 2039 uende katika hali tata ambayo imesemwa, kwa sababu waajiri, waajiriwa na wananchi wanategemea sana mafao yatokanayo na Mfuko huu. Kwa hivyo, tuna haki ya kuweza kuunga mkono ili kuona kwamba Mfuko huu ifikapo mwaka huo hautofilisika kwa sababu zimo haki zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika maeneo makuu ya marekebisho ya Sheria hii.

Mwanzo katika marekebisho inaonekana kwamba kutakuwa na upungufu wa kiinua mgongo kwa asilimia 30, wenzetu wametwambia hivyo na Sheria imesema hivyo. Vile vile kutakuwa na ongezeko la muda wa kuchangia kutoka miaka mitano hadi miaka kumi na tano ili mtu aweze kustahili mafao ya uzeeni, lakini vile vile kutakuwa na ongezeko la viwango vya uchangiaji kutoka asilimia kumi na tano hadi asilimia ishirini iliopo sasa.

Mfanyakazi kutoka asilimia tano atapaswa sasa kuchangia asilimia saba na muajiri kutoka asilimia kumi atapaswa kuchangia asilimia kumi na tatu ili tuendane na viwango vya Mifuko ya Hifadhi katika nchi mbali mbali ikiwemo jirani zetu Tanzania Bara. Lakini vile vile katika maeneo makuu kutakuwa na ongezeko la viwango vya pencheni kwa asilimia ishirini na tano.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mabadiliko haya makubwa ambayo yametajwa yanahitaji elimu kwa wananchi, yanahitaji elimu hususan kwa waajiri na waajiriwa, kwa sababu Waswahili wanasema, "*Fimbo ya ghafla haina mdume*". Lakini vile vile wanasema, "*Mazoea yana tabu*". Lakini kubwa zaidi mabadiliko yoyote yanajenga woga. Lazima tukubali kwamba mabadiliko haya makubwa yatakayojitokeza yanaweza kujenga woga kwa wafanyakazi wetu, waajiri na hata wananchi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, mabadiliko yoyote hata kama yana manufaa mbele yake, hata kama yana neema mbele yake lakini huwa yanajenga woga. Mimi ninasema tu kwamba hapa hivi sasa tuambiwe kwamba Serikali hii ya Mapinduzi iondoke na ikae Serikali nyengine na italeta neema mbali mbali, basi hatupo tayari katika hilo kutokana na uzoefu tulionao wa Serikali yetu na imani tuliyonayo na Serikali yetu. Hata kama tutaahidiwa mazuri vipi kwa Serikali itakayokuja.

Kwa hivyo na wenzetu wafanyakazi, wananchi, kwa mabadiliko haya wanaweza kuwa na woga. Nichukue fursa hii kumuomba sana ndugu yangu Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja kuleta majumuisho, kutumia muda wake kwa kuweza kuwatoa wasi wasi wafanyakazi wetu, wananchi wetu kwa ujumla ili wasishituke sana kutokana na mabadiliko haya, kwa sababu lengo la Serikali ni kuweza kuona kwamba Mfuko huu utakuwa ni endelevu na siyo wa muda.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika suala zima la kipindi cha mpito ambalo nililizungumza jana lakini sikupata muafaka wake. Hivi sasa tuna wafanyakazi ambao wana kima cha chini cha laki moja na nusu. Na Serikali yetu imeahidi kwamba ifikapo mwezi wa Aprili, 2017 wanatarajia kwamba mishahara hii itapanda kutoka shilingi laki moja na nusu hadi shilingi laki tatu.

Lakini Mswada huu baada ya kupitishwa hapa na nina imani kwamba utapitishwa, utasainiwa na Mhe. Rais ili kuanza utekelezaji. Lakini wenzetu hawa ambao wana kima cha chini na wengine katika kipindi hichi baada ya kusainiwa lakini mpaka kufikia mwezi wa Machi ambao wamefikia ule upeo wa kustaafu, watafuata utaratibu upi, huu mpya au ule wa zamani. Hili ningependa Mhe. Waziri atakapokuja aweze kukieleza kipindi cha mpito. Lakini hata wale ambao watastaafu katika kipindi ambacho cha mwaka 2017 na 2018, muda huu utakomea au Sheria hii itaanza kazi katika muafaka upi.

Nije sasa katika Kifungu cha 26(3) ukurasa wa nne wa Mswada wetu. Kifungu hichi ambacho wenzetu wamekizungumza Kamati wameweza kushauri kufanya marekebisho kwamba Waziri ashirikiane au ashauriane na Bodi.

Kifungu kinasomeka, "Waziri ana uwezo wa kucheleweshа mafao ya aina yoyote kutokana na sababu ambazo atajiridhisha kwamba Mfuko hauna uwezo wa kulipa mafao hayo kwa wakati huo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii".

Pamoja na marekebisho ambayo wameyatoa wenzetu lakini na mimi ningeomba kwamba kuwe na muda maalum wa ucheleweshaji huo. Kwa sababu tunarekebisha Mswada huu kwa lengo la kwamba Mfuko uweze kujiendesha vizuri, zile kasoro mbali mbali na matatizo mbali mbali ya kucheleweshewa wafanyakazi mafao yao uondoke. Sasa iwapo hakutokuwa na muda maalum wa ucheleweshaji. Hii ninafikiri inaweza ikawapa hofu wale wastaafu. Kwa hivyo na mimi ninapendekeza hapa kwamba muda uweze kuoneshwa kwamba kutakuwa na muda fulani wa kucheleweshwa kwao.

Nije katika marekebisho ya Kifungu cha 12 (f) kwenye ukurasa wa 59 kuhusiana na kuazima fedha, "Mfuko kuazima fedha kwa njia ya mkopo au kwa njia nyengine kwa lengo la kugharamia miradi".

Mhe. Mwenyekiti, ni suala zuri na lengo ninafikiri ni kuweza kuwekeza ili Mfuko uweze kujizalishia zaidi na hatimaye kuweza kujiendesha vizuri zaidi.

Kabla ya kuingia katika madeni au mikopo kwa sababu mkopo ni deni. Ningeomba sana *ZSSF* iangalie au izingatie vizuri sana katika kuingia katika mikopo. *ZSSF* hivi sasa inatoa mikopo kwa taasisi za Serikali na Mashirika yake na kuna taarifa kwamba hata viongozi na watu wengine wanakopa *ZSSF*. Lakini kwanza sasa tutazame mikopo hii ambayo inatolewa na *ZSSF* sijui kwanza kama ipo kisheria na taratibu na Kanuni kutokana na Sheria hii ambayo tunarekebisha au vipi. Lakini tuweze kujiridhisha kwamba mikopo hiyo ambayo inatolewa urejeshwaji wake upo vipi. Ile ya Mashirika na Taasisi za Serikali na kama kuna watu binafsi vile vile wanaokopa ndani ya Mfuko huu. Tuweze kutazama kwa sababu kama kuna kasoro tuweze kuzirekebisha kabla ya kuja kuingia katika kukopa na huku sisi tukikopesha, lakini urejeshwaji unakuwa siyo mzuri. Sasa hili niwaombe wenzangu wa *ZSSF* liweze kurekebishika.

Lakini nikuulize vile vile Mhe. Mwenyekiti, kwamba taasisi za kifedha zipo ukiacha *ZSSF*, kwa nini mashirika na taasisi za Serikali zikakope *ZSSF*. Kwa nini zisikope mabenki. Hapa kidogo nina wasi wasi. Inawezekana huku kuna bwerera labda. Sasa tuweze kutazama kwa nini taasisi hizi zisikope katika benki, zikakope *ZSSF* ambazo hizi ni fedha za wavuja jasho. Kwa hivyo, ningependa sana kama kuna sera hiyo ya kukopesha itazamwe upya ili kuona kwamba taasisi yetu hii isije ikafilisika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika suala zima la uwekezaji. *ZSSF* niipongeze sana...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakisha dakika mbili.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana.

ZSSF ninaipongeza sana kwa uwekezaji wa miradi lakini niiombe sana miradi ambayo itawekezwa basi miradi hiyo iwe ina tija nzuri ambayo italeta manufaa.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi uliyonipa lakini nimalizie kwa kumuomba Mhe. Waziri, nilipokuwa ninasoma ualimu niliambiwa kwamba mwalimu mzuri ni yule anayetoa mifano. Akija Mhe. Waziri atutolee mfano wa mfanyakazi ambaye alikuwa analipwa shilingi laki tatu hapo mwanzo na keshastaafu na mafao yake ambayo ameyapata na mfanyakazi ambaye atalipwa shilingi laki tatu mshahara wake na mafao yake ambayo atakuja kuyapata baada ya Sheria hii kupitishwa ili tuweze kujifunza kutokana na mfano huo, tuone kwamba mwananchi wa kawaida au mfanyakazi atanufaika vipi katika marekebisho hayo.

Mwisho kabisa nikushukuru Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile niunge mkono Mswada huu upite ili kuweza kuona kwamba tunafungua ukurasa mpya wa kuona kuwa Mfuko wetu huu wa Hifadhi una maendeleo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Rashid Makame. Waheshimiwa Wajumbe naomba nitoe tangazo moja dogo hapa katika ukumbi wetu huu tuna mgeni wa Mhe. Waziri wa Fedha Mhe. Khalid Salum Mohamed ambaye kuwa Ndugu Asgal Mushi Mkurugenzi wa Utumishi, Tathmini na Sera (*SSRA*), yupo hapa. Karibu sana.(*Makofi*).

Baada ya hapo tunaendelea na Mhe. Machano Othman Said nafasi uitumie hiyo.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye uwezo na rehma ambazo sisi zimetufanya tuweze kujumuika kwa pamoja kuzungumzia shughuli hizi za maendeleo ya nchi yetu ya Zanzibar.

Aidha, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji kwa asubuhi hii ya leo kwenye Mswada huu wa marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya mwaka 2005 na kuweka masharti bora zaidi kwa ajili ya ufanisi na usimamizi wa imara wa Mfuko na mambo yanayohusiana nayo.

Pia sina budi kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na timu yake kwa kuifanyia Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunaelewa kwamba kwa ajili ya kulinda maslahi na pia haki za wafanyakazi Mfuko huu ni muhimu sana. Na huko nyuma kabla ya Mfuko huu wafanyakazi ambao waliokuwa wakistaafu kwa hakika walikuwa wakitaabika sana. Ilikuwa lini hajui atapata mafao yake ya kustaafu, pencheni ilikuwa ikiyumba. Lakini kwa juhudi za Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya kuanza Mfuko huu na dhamira kuu, Mfuko huu umeweza kupunguza kero na matumaini yetu kwamba kero zitaondoka kabisa kwa kupitia Mfuko huu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni nchi ndogo sana na ina wafanyakazi kidogo tofauti na majirani zetu wengi. Lakini mfanyakazi ndiyo mfanyakazi, hata wawe kidogo lakini wanazo haki zao za msingi za ajira zao. Kila mara Serikali na sisi Waheshimiwa Wawakilishi na viongozi wengine lengo letu linakuwa moja, katika kuimarisha maslahi ya wafanyakazi zaidi wanapostaafu. Kwa sababu binadamu unapokuwa kazini unaweza kupata fedha ya kula, kwa sababu unakuwa bado unazunguka huku na huku, lakini unapostaafu kazi, na kwa sababu umri wenyewe unakuwa kwenye miaka ya 60, nguvu zako zimepungua na vyanzo vyako vya fedha pia vimepungua. Kwa hivyo, jicho lako kubwa linakuwa kwenye mafao yako ya kustaafu pamoja na pencheni yako.

Mhe. Mwenyekiti, tuko wafanyakazi wa serikali, wapo wafanyakazi wa sekta binafsi, lakini pia kwa mujibu wa marekebisho haya hata *Diaspora* wetu watakuwa na fursa sasa ya kuwekeza kwa kupitia mfuko huu na kuweza kunufaika baadae. Jambo jema hata sisi ambao sio wafanyakazi wa serikali moja kwa moja, ni viongozi, lakini nafikiri mlango uko wazi kuhakikisha kwamba tunaweza tukajiunga kwa masharti maalum ya mfuko.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme wazi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, kwa sababu una mambo mazuri, wakati mwengine kupata mambo mazuri lazima kwanza uumie kidogo, lakini ndio mambo, huwezi ukawa

unaletewa tu pengine, watu wanasema pweza kwenye sahani unakula tu, lakini lazima pengine ukavue au ukanunue sasa ndio mfuko huu.

Mhe. Mwenyekiti, asilimia 15 ya zamani kwamba waajiri 10 na wafanyakazi 5 kwa kuanzia ilikuwa sio mbaya, lakini katika dunia ilikuwa ni miongoni mwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo ilikuwa inatoa kiwango kidogo, kwa hivyo na mapato ya mstaafu yanakuwa kidogo.

Leo mapendekezo twende kwenye asilimia 20, muajiri asilimia 13 na mfanyakazi asilimia 7. Itawaumiza wafanyakazi *take home* yao, lakini haiibiwi hii inawekwa kwa ajili ya maisha ya baadae. Ninaloomba Mhe. Waziri na watendaji wako, wala sina tatizo na wafanyakazi, mimi tatizo langu kwa waajiri, kwa serikali baadhi yao na kwa upande wa serikali zaidi kwa zile taasisi ambazo zinapewa ruzuku, zinakuwa wagumu sana kuwalipia wafanyakazi wao. Mfanyakazi anahisi anakatwa na muajiri wake, lakini kumbe fedha hazipelekwi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwenye sekta binafsi ndio hatari zaidi. Kwanza baadhi ya sekta binafsi zina utaratibu wa kuwashawishi wafanyakazi wao, kwamba pengine analipwa shilingi 700,000/- au 500,000, akubali kwamba mshahara wake ni shilingi 300,000, ili achangie kidogo mfuko huu, lakini pia na muajiri wake na yeye achangie kidogo. Huku ni kumuumiza mfanyakazi. Nawaomba wafanyakazi wa sekta binafsi bora wasikubali, wakubali kusema kiwango sahihi cha mshahara wao.

Pia zipo taasisi binafsi zina wafanyakazi 70, lakini ambao wanalipiwa *ZSSF* pengine ni wafanyakazi 40 na taasisi wakienda wanaambiwa hawa ndio wafanyakazi wetu, ukweli sio huo. Namuomba Mhe. Waziri wafanye utafiti wa kutosha. Suala hili nafikiri wakishirikiana na *TRA* na *PAYE* wanaweza wakabaini uhalisia wa mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, ni huzuni kubwa, baadhi ya wafanyakazi wanafanyakazi mpaka muda wao unafika wa kulipwa, lakini wanaambiwa fedha huku hazijaletwa kwa miaka minne au mitano, inakuwa ni majanga kwao na inaleta adha kubwa kwao na familia zao pia, na muda wa umri unakuwa umeshakwenda sana.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tumuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ajitahidi sana kuweka mambo sawa. Kwa bahati nzuri kuna miaka na yeye alikuwa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hii *ZSSF*. Kwa hivyo, nina hakika Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, huu mfuko

anaujua nje ndani, kwa sababu alishawahi kuutumikia kama Mwenyekiti wa Bodi. Sasa hivi ni Waziri wa Fedha na Mipango, hivyo atakuwa na nafasi zaidi ya kuona na kutambua mapungufu ambayo kwa muda mrefu yalikuwa kwenye mfuko ule.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la asilimia ya malipo ya mwisho, asilimia 36 ya mshahara. Mhe. Mwenyekiti, suala hili na mimi naliunga mkono. Kamati imesema inawezekana ikawa mzigo kwa waajiri, lakini pia mzigo kwa mfuko wakati wa kutoa mafao ya watu hawa. Wengi wa wafanyakazi wetu wanapata kipato cha chini sana, yaani kwa dunia ya leo kupata kiinua mgongo cha milioni 20 kwa mfanyakazi anaumia sana, kwa sababu wengine hata hiyo milioni 20 hawafiki. Lakini nafikiri mliwahi kumsikia mtu mmoja kasema wao wanafika mpaka milioni 700 au 800 sio mfuko wa hifadhi. Mimi nasema asilimia 36 angalau itatusaidia kuwafanya na wao wafanyakazi wawe na kipato cha kuondokea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini inawezekana isiwe tatizo sana. Kwa sababu kila kiwango cha mshahara kikipanda maana yake na wewe makato yako asilimia 20 yanapanda. Sasa ile hoja ya kwamba mshahara ukipanda mfuko utaumia, mimi naona siioni sana mantiki yake, kwa sababu mshahara ukipanda asilimia 20 yako, kama ulikuwa ukipata shilingi 300,000 basi asilimia 20 ya 300,000 inatofauti na inabadilika. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba hii asilimia 36 ndio tuanze nayo ili wafanyakazi wetu wafaidike.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine na hili mifuko mingi inafanya. Kwa sisi watu wa kada kama hii ya waheshimiwa, mifuko inatoa mikopo katika chanzo chake cha fedha chengine. Wanawakopesha mfano waheshimiwa kwa riba wanayokubaliana na malipo wanayokubaliana, lakini pia wanawapa uanachama wa hiyari ambao pia unaweka *deposit* kwa kila mwezi.

Kwa mfano, ukikopa katika mfuko wa hifadhi, ukiachilia mbali ulipaji wa deni lako, lakini kila mwezi kwa miezi yako 60 unalipa, mfano unazo shilingi 400,000, au 500,000, ukimaliza deni na baada ya muda wako, fedha zako zile unarejeshewa pia utakuwa umesaidiwa katika shughuli hii.

Kwa hivyo, naomba na mfuko huu wa *ZSSF* uanze kama haujaanza utaratibu huu kwa kuwafikiria, na hili linaweza kuwa na changamoto na taasisi za fedha nyengine, badala ya wao kwenda kuweka fedha zote benki kwa riba ndogo, ukiwakopesha watu ambao wana uhakika riba yako pengine inaweza kuwa kubwa zaidi kuliko ile uliyoweka wewe na benki mliyokubaliana, lakini ikawa

ndogo kwamba hawa waheshimiwa kuliko kukopa benki, hili linaweza likasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niombe kwamba tunalo tatizo sisi hapa Zanzibar na Tanzania kwa jumla, tatizo letu wanafunzi wetu wa vyuo vikuu, sasa hivi ni wengi kuliko uwezo wa serikali kupitia Bodi ya Mikopo kuwakopesha, hatima yake inakuwaje. Hatima yake inakuwa ama Mhe. Mwakilishi na Mbunge, ama wazazi wengine wakauze ng'ombe au wauze kitu chengine wawasomeshe watoto wao.

Mimi nina ushauri kwamba tuuangalie mfuko wetu zaidi kwa wafanyakazi wa serikali wanaotaka kusoma, badala ya kukopeshwa na mfuko ule wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, basi wafunguliwe dirisha la kukopa kwa kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na riba yao isiwe sawa na ile ya benki, lakini wahakikishe kwamba wanalipa na pengine hii inaweza kusaidia mpaka Waheshimiwa Wawakilishi wakawachukulia dhamana wanafunzi wawili au watatu katika majimbo yao kwa mikopo na wakakatwa wao fedha moja kwa moja zikawasaidia vijana wetu kusoma, kuliko kumtarajia Waziri wa WEMA awasomeshe wanafunzi wote inaweza kuwa ni ngumu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano tuko wajumbe 80 humu ndani, kama utakubaliwa kukopa kila mmoja akiwachukua wanafunzi 5 kuwasomesha, ina maana tunaweza tukawa na wanafunzi karibu 400 tumewasomesha kwa kupitia mfuko huu na nafikiri tunaweza kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, dakika mbili malizia.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, ungenipa dakika 5, maana wachangiaji wenyewe kidogo. Lakini sawa naheshimu muda wako.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 7(3) ambacho kamati imeshauri Mhe. Waziri ashauriane na bodi.

Mimi nina hofu tu kidogo ya sheria yenyewe ilivyo ya mfuko huu. Kwa kawaida mamlaka ya waziri ni makubwa sana kuliko bodi. Labda mimi niseme kwamba labda baada ya kushauriwa na bodi. Lakini ukisema washauriane na bodi, kama upande mmoja haukukubali inakuwa shida, kama bodi haikukubali, inawezekana hakukuwa na makubaliano hili linaweza kuwa na shida. Mimi nafikiria bodi imshauri waziri ili waziri atoe maamuzi ya kwamba huyo mtu asilipwe kwa wakati unaohusika. Haya ni mawazo yangu tu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuheshimu agizo lako, kwamba mfuko wetu na mifuko yote ilivyo inaingia katika uwekezaji kwa kupitia miradi, na mabadiliko ya kiuchumi ya dunia pia yanaathiri sana uwekezaji katika mifuko. Namuomba sana Mhe. Waziri na mfuko huu, wawe makini katika maeneo ya uwekezaji. Msiwekeze katika maeneo ambayo baadae hayawezi kurejesha mtaji wetu na hayana tija kwa nchi. Ni matarajio yangu kwamba watakuwa wanafanya utafiti mzuri, watakuwa wanashughulika vizuri na wataweza kuusaidia mfuko huu. Ni matumainio yangu kwamba mfuko huu hauwezi kuyumba na utasonga mbele.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa mara nyengine tena niseme kwamba mimi naunga mkono mswada huu wa marekebisho ya sheria hii kwa asilimia mia, na nawaomba na waheshimiwa wenzangu tuuchangie ili kuuimarisha mfuko wetu huu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Machano Othman, sasa ni zamu ya Mhe. Dk. Makame Ali Ussi Mwakilishi wa Jimbo la Mtopepo, na baadae atafuatia Mhe. Mohamed Ahmada Salum (Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Dk. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi niwe mmoja kati ya wachangiaji wa mfuko huu adhimu, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Kwanza niseme tu kwamba mfuko wa hifadhi ya jamii kwa maana pana, unachukua mambo mengi sana, ikiwemo hata *social control*, ikiwemo hata kufuatilia mienendo ya watu wanaozeeka, ufuatiliaji ukuaji wa *population* yetu na tabia zao, kwa sababu inachukua mpaka mambo ya usalama na kadhalika, ndio maana ya *social control.* Lakini kwa sababu ya mfuko huu hapa leo ambao unachukua masuala ya waliostaafu na kadhalika.

Kwanza ningependa sana nianze kuupongeza huu mfuko. Ni mfuko mzuri ambao kwa kweli utasaidia jamii sana huko mbele inakokwenda wakati ambapo nguvu zinakuwa zimeshawapungua, hususan wafanyakazi kwa maana ndio *coverage* kubwa hapa.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nataka niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia kabla sijachangia. Nasema suala lolote linalohusiana na jamii na hasa hii ya hifadhi ya jamii, lazima liende sambamba na kuwapatia vitu ambavyo vitaleta usalama kwao. Kimoja kati ya hiki ambacho ni muhimu sana ni nyumba za kuishi hapa wanapomaliza wengi wanaishi katika nyumba nzuri sasa hivi,

wakati huu wakiwa kazini wakipata pesa mbili tatu. Lakini pesa mbili tatu zile zikiisha wakianza maisha mapya, basi nyumba zile zinaanza kupoteza hadhi yake na zinakuwa nyumba ambazo kwa kweli hazifai au haziko katika hali nzuri ya kuishi binadamu.

Kwa hivyo, napongeza sana hizo nyumba zinazojengwa sasa hivi kwa ajili ya wananchi ambao watapatiwa. Pia ningependekeza sana mfuko huu uanze kuwakopesha wananchi, hususan hao wafanyakazi, wakopeshwe fedha japo nusu ya kiinua mgongo chao, ili waweze kuanza kujenga nyumba, iwe maalumu kwa ajili ya ujenzi ambao ujenzi huo au nyumba hizo zitakuja kuwasaidia wenyewe hapo baadae watakapostaafu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ningependa sana nipendekeze. Kuna vijana wengi hawana kazi wako mitaani. Sasa tukiangalia *social security* hatutaki vijana hawa waingie kwenye majanga ambayo kwa kweli hayana manufaa, wanaifanya hata jamii isiwe na usalama katika kuishi kwao. Kwa hivyo, nadhani mfuko huu pia ungeangalia uwezekano wa kuwakusanya hawa vijana kwa kushirikiana na uwezeshaji, wakawakusanya vijana na kuwapatia kazi ambayo inaweza ikawaendeshea maisha yao ya hivi sasa na ya baadae.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo napendekeza sana ni kwamba kuna majengo. Kwa mfano kule Mkokotoni, jengo lile lililokuwa la mkoa zamani, jengo lile lingewafaa sana *ZSSF* wakalichukua jengo lile, halafu wakawaorodhesha wavuvi, pale kuna wavuvi wengi sana, wakawaorodhesha wavuvi wakawaingiza kwenye mfumo huu na wao wakanufaika na mfuko huu. Jengo lile lina historia ambalo kama litaweza kukarabatiwa na *ZSSF* wakalitumia kama ofisi yao, basi mnaweza kuongeza hata mapato yao.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna sehemu ambazo wanaweza kujenga *ZSSF*, wengine wamesema viwanda. Mimi nasema hata wakitengeneza *boat yard*, kwa mfano hapo Mkokotoni na kwengine, maegesho ambayo wanaweza wakaegesha boti wakalipa angalau shilingi 200/- tu kwa siku. Kwa sababu siku hizi mtindo unaofanywa maboti yao wale hawana pa kuyaweka, yanaelea asubuhi pengine akienda kachelewa limeshaanza kuopolewa, ulitoe pale lilipoopolewa kulipeleka baharini. Sasa kama kuna mahala pa kuegesha saa yoyote mtu anaweza kwenda kuvua. Sasa kama wataweza kujenga sehemu ya kuegesha maboti yake wakawa wanalipisha hata shilingi 200/- kwa siku, basi pia mfuko huu ungeweza kutanuka na ukapata mafao zaidi, hasa ukizingatia kwamba fedha zinazolipwa na wachangiaji ambao ni wafanyakazi ni ndogo kuliko vile ambavyo mfuko unatarajia kukua.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho natoa msisitizo tu kwamba ni vizuri *ZSSF* ikajikita kwenye mambo ya viwanda kama walivyochangia wenzangu, na kwenye mambo mengi ya ujasiriamali, ili waweze kukusanya mapato makubwa zaidi.

Baada ya kusema hayo, mimi sikutaka kuchangia sana kwa sababu huu mswada ni mzuri, hauna matatizo sana, isipokuwa ni kutoa mapendekezo tu ili kuuboresha. Kwa hivyo, baada ya mchango huo naomba kukushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii kuchangia angalau kwa uchache tu mswada huu, ambao kusema kweli tokea jana tumepata elimu kubwa sana kutoka kwa Mhe. Waziri na bodi yake yote ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Kusema kweli elimu ile tumepewa ya kutosha, isipokuwa hivi sasa kutokana na wajibu wetu, basi na mimi sina budi kuchangia kidogo tu kwa vile na sisi pia tunaingia katika mifuko hii, ama hivi sasa au hapo kabla na hata baadae.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyochangia wenzangu, nitapenda vile vile nichangie katika kifungu hiki cha namba 26(3), kuhusu uwezo wa Mhe. Waziri kwa kuweza kucheleweshe ulipaji.

Mimi sina tatizo na suala hili, isipokuwa tu na mimi nina mapendekezo kidogo kwamba kabla ya kufanya hayo maamuzi basi kwanza Bodi ikae na baadae wampelekee Mhe. Waziri, na Mhe, Waziri baadae ndio aamue. Lakini hata hivyo na yeye Mhe. Waziri aweke muda maalumu kwamba hili suala lisichukue muda sana kama unavyojua huu ndio uhai wa mtu yeyote, baada ya kufanya kazi kutumikia nchi yake kwa muda mrefu anapokuwa kazini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo nije kifungu cha 44 sehemu hiyo hiyo ya pili kuhusu Waziri kwa kushauriana na bodi anaweza kutayarisha kamati za kuanzisha hii mifuko. Kusema kweli hili suala ni zuri sana, kama tunavyojua kwamba mifuko hii inahitaji mitaji ili iweze kujiendeleza zaidi na vile vile baadae kuweza kuwalipa vizuri watu wake wale kwenye viinua mgongo na pencheni vile vile. Sasa hili ni wazo zuri sana na mimi naliunga mkono kabisa, isipokuwa tu mimi ningependa kuchukua nafasi hii kumshauri Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba inatolewa elimu ya kutosha kuhusu namna gani hawa watu wanaweza kuingizwa kwenye mifuko hii ya hiyari, kwani sote tunajua kwamba mtu huwezi kujua umuhimu wa kitu mpaka upate matatizo.

Na hii mifuko ya hifadhi inasaidia sana katika maisha ya baadae hasa baada ya mtu kushindwa kwa aina yoyote ile au kustaafu kufanya kazi, kwa hivyo, mimi nitamuomba sana itolewe elimu katika upande huu kwani wananchi wengi wa Zanzibar bado hawajawa na elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa hii mifuko, kwani hata katika sekta binafsi utakuta kwamba kama alivyosema Mhe. Machano baadhi ya waajiri kwa makusudi kabisa huwa wanakwepa kupeleka taarifa sahihi katika mifuko hii, kwa ajili tu ya kuona kwamba labda kile wanachompa mwajiriwa wao kwamba ni moja ya sehemu ya kutoa pesa mfukoni mwao.

Kwa hivyo inatakiwa na wao pia wapewe elimu kwamba hii ni vile vile unamjengea muajiriwa wako kufanya kazi kwa bidii na kwa uzalendo zaidi, na vile vile kuongeza tija, kile ambacho umempangia akizalishe, kwa hivyo mimi nitatoa ushauri sana kupitia Mhe. Waziri wa Fedha ahakikishe kwamba hasa sekta binafsi kwamba, japo baadhi ya wenzangu wamesema kuna baadhi ya sehemu za taasisi za Serikali lakini mimi nina imani kubwa sana zaidi katika sekta ya binafsi basi wahakikishe kwamba wanapewa elimu ya kutosha, kwamba hicho wanachokifanya vile vile wanakifanya katika kuendeleza tija kwa mfanyakazi na vile vile kwa yeye kitamsaidia kwake baadae katika kuongeza tija katika kampuni yake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuelezea hayo vile vile nije katika jadweli la kwanza kuhusu viwango vya michango, mimi sasa hapa vile vile nimshukuru Mhe. Waziri kwani kiwango hichi cha asilimia 13 kwa muajiri na asilimia 7 kwa muajiriwa ni kiwango kizuri sana, lakini vile vile kama nilivyosema mwanzo, kwamba katika sekta binafsi bado nina wasi wasi kuhusu kwamba wasifanye ipasavyo kwa ufanisi. Kama ilivyotokezea kwamba hivi sasa wanakuwa na wafanyakazi lakini wafanyakazi wale hawajui haki zao, kwa hivyo wanatumia fursa hiyo ya kutokujua wale wafanyakazi haki zao kwamba katika mifuko hii ya hifadhi ina aina fulani vile vile ya kuweka akiba uzeeni, kwa hivyo wanakuwa hawapeleki kule.

Kwa hivyo mimi nitaomba sana katika hili vile vile wawe karibu sana na watu wa sekta binafsi, kwani baadhi ya wakati utakuta wafanyakazi wa Hifadhi ya jamii wanakwenda mpaka kwenye kampuni au shirika fulani la sekta binafsi, lakini wakifika kule wanaridhika na taarifa wanazopewa na muajiri bila ya kuwadadisi wale waajiriwa kama kweli wanalipwa mishahara ile au je, ile mishahara inapelekwa sehemu husika.

Katika mifuko mingine hasa kule Tanzania Bara kuna wigo mzuri sana ikiwa wewe ni muajiriwa basi kila baada ya muda miezi mitatu au miezi sita

unaletewa ile jadweli ya kuonesha kwamba wewe mpaka muda huu umeshachangia michango mingapi na fedha zako ni hizi, kwa hivyo inakusaidia wewe kujua kwamba kweli muajiri wako anapeleka fedha kunakohusika na ipasavyo.

Kwa hivyo mimi nashauri kama sisi katika mifuko yetu ya Hifadhi ya Zanzibar hatuna jambo hili mpaka muajiriwa mwenyewe aende akaulize basi mimi nashauri sana tuandae utaratibu wa wenzetu Bara, ambao kila baada ya muda wanakuletea kwa njia ya boksi au pale pale kwa muajiri wako, kujua kwamba michango yako imeshafikia kiasi gani na wewe hifadhi yako kwa muajiri wako. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, mimi kama walivyosema wenzangu nitaomba vile vile mfuko wetu huu uangalie kwa upande zaidi wigo wa kutanua uwekezaji wake zaidi, wasitegemee kuwekeza katika mambo ya nyumba tu, vile vile waangalie ile biashara ambayo kwa kiasi kikubwa itaweza kuwaingizia tija waajiriwa wao, na vile vile kuweza kuwaingizia tija wale ambao wanafaidika na hii mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mimi nina mfano mzuri sana kwa nchi nyengine Malaysia, Bangladesh na China wamepiga hatua sana kutumia mifuko hii ya kazi katika kuhakikisha kwamba mitaji ya mifuko hii inaongezeka zaidi na baadae kuweza kuwasaidia waajiriwa wa mifuko hii kupata faida au pencheni nzuri zaidi hapo wanapokuja kustaafu. Kwa hivyo mimi nitatoa wito sana kwa Mhe. Waziri, hili aliangalie kwa upana wake kwani litasaidia sana, baadae wananchi wengi kuweza kujiunga katika mifuko hii ima kwa hiyari au kwa kutumia utaratibu wa lazima kwa makampuni au kwa taasisi za Serikali.

Mwisho kabisa kabla ya kuunga mkono hii hoja mimi ningependekeza katika hii wenyewe wanayosema Dkt. Khalid Salum Mohammed badala ya kuandika DR badala yake tuandike Kiswahili Dkt. hii itakuwa vizuri zaidi, kwa sababu huu ni mswada wa Kiswahili na tutakapoandika DR. maana yake tunatumia zaidi neno la Kiingereza.

Mwisho kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Malindi naunga mkono hoja hii, kwani ni hoja muhimu sana katika mustakbali wa watu wetu, na nina imani kubwa sana na Wawakilishi wenzangu nao wataiunga mkono hii hoja ili kuendeleza mfuko huu kwa maslahi yetu na nchi yetu kwa jumla. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia mswada wetu huu wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii No. 2 ya mwaka

2005, na mimi kabla ya kuendelea nichukue fursa hii kuunga mkono Mswada huu kwa ukamilifu wake.

Sasa basi nachukua fursa hii baada ya kusoma Mswada kwa kina nimeufahamu na nimeona kwamba umekuja wakati unaofaa kabisa, mimi sitozungumzia vifungu moja kwa moja, lakini nitazungumzia uhalali wa Mswada huu, mara nyingi huwa tunaagiza kwamba ni muhimu maamuzi tunayofanya yakawa yanafanywa katika misingi ya ushahidi na ndio Mswada huu ulivyo.

Tafiti zaidi ya tatu zimetumika kutafiti namna bora ya kuendesha mfuko huu wa Hifadhi na imeonekana kwamba katika tafiti zote hizo kwamba ni bora tukafanya mageuzi kidogo ambayo ndio haya Mhe. Waziri ameyaleta ili kuimarisha, na ingetosha tu kusema tumeupitisha kwa sababu wengi wetu hatujafanya utafiti kwa hivyo tutakuwa tunachangia tu hapa na pale. Kwa hivyo niseme kwamba Mswada huu tunauunga mkono kutokana na kwamba kuna ushahidi wa kisayansi kabisa kwa haya mapendekezo ambayo yameingizwa katika Mswada huu.

Jambo jengine ambalo nataka kusisitiza kwamba wakati tukiupitisha Mswada huu hapa hapo baadae na ukapitishwa ukawa sheria, kwamba mapato yatakayokusanywa mwaka hadi mwaka yatumike kwa faida kubwa kabisa, kwanza kwa kuutunza mfuko wenyewe huu, isijekuwa ile hadithi ya punda kula msoji wake ni kwamba utumike katika kuimarisha siku hadi siku na uwe mfuko bora baadae, sina hakika labda dira ya mfuko wa jamii inasemaje, lakini tunataka iwe ni mfuko bora kabisa katika kanda hii ya Afrika ya Mashariki na Kati.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba faida itakayopatikana katika mfuko huu pamoja na kuwasaidia wastaafu hapo baadae, lakini katika kipindi hichi cha muelekeo wa huko mfuko huu ufikirie namna ya kuwasaidia au kuwakopesha vyovyote itakavyokuwa katika kipindi hichi, kabla mtu hajafikia umri wake wa kustaafu, kama wanavyofanya baadhi ya mifuko huwa wanatoa *incentives* mbali mbali, kwa hivyo nashauri kwamba mfuko pia nao ufikirie namna ya kuimarisha zaidi hizi *incentives* kwa ajili ya kuwapa matumaini zaidi wanachama wake.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kwa kuwa jamii ina matarajio ya mfuko huu, na hapa mazungumzo yetu na wawakilishi ambayo yameanza kutolewa kuna wanaosema kwamba wangependa mfuko huu ujiendeshe kibiashara, kwa maana kwamba labda ufanye kazi kama taasisi za benki, na kuna maoni

yanayosema kwamba labda mfuko huu usaidie pia shughuli nyengine za kijamii, kwa mfano kukopesha vijana, kukopesha wanafunzi n.k.

Kwa hivyo hapa kuna mawazo mawili yanayogongana kwa kweli, lakini kwa maoni yangu mimi nahisi kwamba mfuko huu uangalie mambo yote mawili, uangalie shughuli ambazo zitaleta faida kwa mfuko, lakini pia uangalie shughuli nyengine ambazo hazina *return* kubwa lakini zina manufaa makubwa kwa jamii nazo lazima ziangaliwe, nazo ni hizo shughuli za upunguzaji umasikini, shughuli za elimu, shughuli za kimatibabu nazo pia zitizamwe japokuwa *return* zake sio kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, tukifanya hivyo nadhani majina yetu yatakumbukwa hapo baadae katika historia, kwamba tumeitendea haki jamii yetu, tukilenga tu moja kwa moja katika masuala ya kuleta faida, jamii itatuelewa zaidi kwa sababu yale mambo tunayoyafanya watakuwa wanayaona kwa macho yao, kwa hivyo hilo ni suala muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kwa kawaida sisi binadamu tuna desturi ya kuhofia mabadiliko au kuogopa mabadiliko, ni sawa kwa sababu hatujui huko mbele yatakuwaje, tutakuwa kama tulivyo, tutafaidika kama tulivyo, au tutaathirika. Sasa hofu hii lazima iondolewe, na njia moja ya kuondoa hofu ni kuelimisha jamii, na njia bora kabisa ya kuelimisha jamii ni kuishirikisha jamii, lazima tuishirikishe jamii ili iondokane na hofu na wawe na matarajio mazuri na mema kwa kuweko mfuko huu.

Na Wataalamu wengine wanasema kwamba ili kuleta mabadiliko, na kwa kuwa watu wanahofu mabadiliko, basi ni vyema kidogo ukatumia nguvu, lakini katika nyakati hizi nguvu tunayoisema zaidi ni nguvu hii ya elimu, nguvu ya kufunza jamii. Lakini suala tutafunza wapi, kuna nyakati tofauti, kuna sehemu tafauti za kukuza jamii lakini vyema tukafikiria njia bora zaidi ya kuelewesha jamii, tunaweza tukaanza katika maskuli, tunaweza kuja katika sehemu nyengine mbali mbali za jamii, lakini kwa kweli lazima jamii tuielimishe.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba wakati wa utekelezaji wa sheria hii maamuzi yoyote ya miradi ambayo itafanywa na taasisi hii lazima nayo iende kwa mujibu wa tafiti. Watendaji wa mfuko wasijaribu hata siku moja kufanya maamuzi kwa dhana tu, kwa fikra tu, nadhani lazima wafanye kazi wafanye maamuzi ambayo yatafanywa kwa ushahidi kama maamuzi ya kuleta Mswada huu yalivyofanywa. Kwa hivyo miradi ipo, waisome kwa makini, watafiti kwa makini, watizame faida yake kwa nani, watizame hasara yake kwa

nani halafu baadae hapo ndio watoe uamuzi. Tukifanya hivyo basi nadhani tutapata matunda tunayoyatarajia.

Kwa kusisitiza zaidi kwamba Mswada huu umefanyiwa utafiti wa kutosha hata uwiano wa asilimia inayopendekezwa, asilimia 13% kwa muajiri na asilimia 7% kwa muajiriwa nayo pia haikufanywa kiholela, imefanywa kwa uchunguzi kamili, kwa hivyo haina shaka na kwa maana hiyo mimi naiunga mkono *hundred percent*.

Kwa hivyo, kwa niaba ya wapiga kura wangu katika Jimbo la Mkoani naunga mkono Mswada huu. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu naona hili suala linagusa sana pia kwenye Wizara yangu ambayo kuna masuala ya ujasiriamali, na pia kwa ajira za kazi watu wanapomaliza namna gani waweze kuendeleza maisha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu wote waliochangia kwa nia ya kuunga mkono Mswada huu.

Pia napenda niongezee kitu kusema kwamba Mhe. Shihata kasema karibu mawazo mengi ambayo nilikuwa nimeyazungumza pamoja na wengine waliokuwa wameshasema, lakini bado nilikuwa nasisitiza suala zima la kuona kwamba wajasiriamali au watu wanaofanya kazi binafsi waweze kutafuta utaratibu gani wanaweza kuchangia, wanaweza kuweka mifuko yao katika huu mfuko wa *ZSSF*, nchi nyengine wanathubutu hata kuchangia hata ma- *house girls*, watu wanapofanya kazi majumbani, akija mfanyakazi kufanya kazi kwanza inabidi alete cheti kutoka kwa muajiri wake wa awali, na ile inasaidia kuona kwamba unapokea mtu ambaye ni muaminifu na ambaye hajatoroka katika eneo lake. Lakini bado katika mshahara utakaompa unamkata kiasi kidogo cha kumuwekea akiba, na kile kinampa nidhamu ya kuwa na mawazo ya kuona kwamba saa yoyote naweza kuondoka, kwa hivyo kunakuwa na mikataba.

Pia sasa hivi kumekuwa na wimbi kubwa la masuala ya ujasiriamali, na ujasiriamali sasa hivi umekuwa ni wa kisasa, sasa hivi nimekuwa nikifungua maeneo mbali mbali ambayo wajasiri amali wanakwenda kimtandao, wamefikia kiasi cha kusema kwamba wana wazo la kutaka kuanzisha benki zao wenyewe. Ni jana tu nimekwenda kufungua mtandao mmoja ambao wajasiri amali kutoka sehemu mbali mbali; Tanga na Zanzibar, wameweka akiba kiasi

cha bilioni 8 na ili uanzishe benki unapaswa kuwa na bilioni 15, kwa hivyo sasa hivi wana bilioni 8 kitu kinachotakiwa kufanywa ni bilioni 7 tu. Na ukiangalia miradi mingine wana pesa nyingi sana za kutosha, sasa hii itasaidia sana wale wote wanaohisi kwamba waache kuwa na mawazo ya kwamba ajira mpaka aajiriwe na Serikali.

Lakini kama watakuwa na uhakika wa kuweka mfuko na kuweka akiba zao na wao siku moja wakapata pencheni au wakapata mfuko wa pamoja kwa ajili ya kuendeleza maisha yao uzeeni itakuwa ni jambo zuri sana. Sasa ninachosisitiza hapa ni kuomba watakaokuwa wanahusika kuhakikisha kwamba wanatoa elimu ya kutosha, kuna tabia ya kuwa na vipeperushi wanatoa wanaviweka sawa kwa wale wachache watakaoweza kuwafikia. Lakini kuna wengine hata namna ya kusoma vipeperushi hawana.

Kwa hivyo ningeshauri kabisa watu wa *ZSSF* wajitahidi kwenda kuhakikisha kwamba, pamoja na Wizara zinazohusika na masuala ya biashara, ujasiri amali na wengine, ili waweze kuhakikisha watu wale wanafikiwa na ile elimu na wanaweza kuwa na moyo wa kuweza kuweka miradi, kitu ambacho kitatoa hofu hata vijana wetu wanaomaliza vyuoni, huwezi ukaajiri wote na imekuwa ni vizuri sana sasa hivi ujinga Zanzibar umetutoka, isitutie hofu kubwa sana kusema kwamba kila anayetoka chuoni au kumaliza kazi lazima aajiriwe, tunafurahi kwamba hata asipoajiriwa, lakini hawa wasomi walioko ndani ya nchi ndio watakaokuwa na mawazo ya kisasa ya kuanza kufungua mbinu mpya za kuweza kuyakabili maisha, kwa hivyo ni jambo zuri kwa upande huo.

Pia kuna suala zima la watu wa kima cha chini, mshahara lakini sio ile mishahara mikubwa kwa sababu tunapishana katika mishahara, kuna wale ambao wanakwenda kuanza miaka miwili, mitatu ijayo anataka kwenda kupumzika, lakini kutokana na harakati inakuwa ni tatizo. Kwa mfano mimi nimekuwa sili na mwalimu, kwenye pencheni unayopewa ni mwalimu inakuwa haitoshelezi sana wewe kwenda kuanza maisha mengine mapya, na zile harakati za walimu kuhangaika huku na kule huna nafasi ya kituo ya kusema kwamba una mipango nyeti ambayo inaweza kukusaidia kwa ajili ya kuweka akiba.

Sijui inawezekanaje, lakini ni vyema pia ikiwezekana wapewe *package* mapema kabla najua ni jambo ambalo linaweza likazungumzika na kuangalia ni utaratibu gani,wanaposema watatoa mikopo kwa watu mbali mbali ya masomo pia na hawa wa maisha ya kawaida basi wapewe ili iweze kuwasaidia kuona kwamba jinsi gani nitafanya. Najua Serikali ina nia nzuri na ndio mipango ya miradi kama hii inatokezea sasa hivi *ZSSF*, inajenga nyumba ambayo

tunaamini kabisa wale wenye uwezo watanunua, lakini hawa watakaokuwa wamechajishwa katika namna gani ya kuweza kuweka pesa vizuri wanaweza kuwa na uhakika wa kuweza kusaidia kwamba wanapata fedha za kudumu.

Na hii pia inaendelea kutitia moyo, kwamba watu kadri walivyokuwa hawana hofu ya kipato maisha yanaendelea yanakuwa ni mengi zaidi, wanaishi wanaacha mikandamizo kwa kukata tamaa mapema, kwa hivyo watapata nafasi ya kuweza kufaidi ule mfuko wa pencheni uliteuliwa na Dkt. Ali Mohamed Shein, ambao sasa hivi kwa kweli japokuwa tulikuwa na mambo mengi ambayo tumeyarekebisha na tunaendelea kuangalia utaratibu utakaokuwa ni mzuri, ili kila mmoja anayestahili kupewa apewe. Lakini pia hawa watu ikiwa watakuwa na mipango mizuri itakayowasaidia kiwango cha kufa mapema kitapungua na sisi ndio lengo letu, hatutaki watu wawe wanazeeka siku mbili mtu ana afya yake anapotea kwa sababu ya majukumu ya watoto yanaendelea kubakia kwa watu wachache, lakini kama watu watakuwa wamehamasika na wana uwezo kipesa, inakuwa ni njia rahisi zaidi.

Kwa hivyo, napenda nichukue nafasi hii kuunga mkono Mswada huu asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nianze kwa kumshukuru *Allah* kwa kutupa uhai na afya, lakini vile vile nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Mswada huu.

Aidha naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake wote kwa kuona umuhimu wa kuleta Mswada huu kwa ajili ya kuboresha huduma za jamii za mfuko huu wa hifadhi ya jamii, naomba nikiri kwamba Mswada huu umekuja wakati muafaka, ambapo uimara wa maslahi kwa wafanyakazi wa kada zote na makundi mbali mbali utaimarika, hasa katika sekta zisizo rasmi, hii ni hatua kubwa na ya kujivunia kwetu kwa faida ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mengi yamezungumzwa nitajitahidi sana nizungumze kwa ufupi sana. Mswada huu wa Sheria umeona umuhimu wa sekta binafsi kuwawekea utaratibu mzuri wa uchangiaji na hatimaye wafanyakazi wa makundi haya ya ajira zisizo rasmi watafaidika sasa hivi. Aidha, naomba nichukue nafasi hii tena niendelee kuipongeza Wizara hii kwa kulifikiria kundi hili kubwa la wajasiri amali ambao wengi wao ni wanawake, kwa kuweka utaratibu mzuri ambao utaleta tija na misingi mizuri kwa maisha ya baadae.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Baraza lako hili naomba niwaombe sana wananchi kwa kuweza kutumia fursa hii iliyowekwa ipasavyo kwa faida yao ya baadae. Mhe.Mwenyekiti naomba sana kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, na niwaombe pia wajumbe wenzangu waweze kuunga mkono hoja hii ili mswada huu uwe Sheria kamili na Wazanzibari kwa ujumla wao waweze kufaidika na sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti naomba kuunga mkono hoja*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa kwa sababu wachangiaji wetu wa leo wamemalizika, tutamuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu, kwa sababu bado muda upo, na kwa sababu Waziri anahitaji muda kidogo kwenda kuonana na watendaji wake ili aweze kuja kujibu hoja jioni.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kama ambavyo umetangulia kusema kwa kuwa wachangiaji wa Mswada huu wamemalizika, na kwa kuwa muda bado tunao, sasa niombe kutoa hoja ya kutenga kando kanuni ya muda, ili tuahirishe kikao hichi na tumpe fursa Mhe. Waziri wa Fedha akajitayarishe na aje kufanya majumuisho jioni.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja ya kutenga kando kanuni ya muda. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa, wanaounga mkono hoja wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 6:18 Mchana Baraza liliahirishwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, lakini pia nimshukuru Mhe. Mwenyekiti, aliye *chair session* asubuhi kwa kuendesha mijadala na hoja za Wajumbe kwa umakini mkubwa.

Pili Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa michango yao kama nilivyosema pale asubuhi. Lakini vile vile nimshukuru sana Makamo Mwenyekiti wa Kamati hiyo na Wajumbe wote kwa michango yao, niseme tu maoni ya kamati tumeyapokea na tutayazingatia ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja niliyoiwasilisha ilichangiwa na Wajumbe 14, Wajumbe 10 walichangia moja kwa moja lakini Wajumbe wanne walichangia kwa maandishi. Kwa ruhusa yako naomba niwatambue waliochangia wote.

1) Mhe. Hamida Abdalla Issa Viti maalum ambaye alichangia kwa niaba ya Mhe. Yussuf Hassan Iddi.
2) Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
3) Mhe. Rashid Makame Shamsi
4) Mhe. Machano Othman Said
5) Mhe. Makame Ali Ussi
6) Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
7) Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji
8) Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
9) Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Waliochangia kwa maandishi ni:-

10) Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
11) Mhe. Zulfa Mmaka Omar
12) Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
13) Mhe. Shamata Shaame Khamis; na
14) Mhe. Bahati Khamis Kombo

Mhe. Naibu Spika, jambo moja kubwa lililochangiwa na Wajumbe wengi kidogo ni suala la taaluma.

Mhe. Ali Suleiman aligusia suala la taaluma, Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na Mhe. Rashid Shamsi pamoja na Mhe. Mohammed Ahmada wote walizungumza suala la taaluma, wanataka taaluma zaidi itolewa kwa wafanyakazi katika sekta ya umma, lakini vile vile katika sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ili waweze kuelewa marekebisho yaliyofanyika au yanayotarajiwa kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Niseme tu kwamba mfuko ni kawaida yake kutoa taaluma na imekuwa ikitoa taaluma kwa nyanja mbali mbali na kupita njia tofauti moja imekuwa ikitoa mafunzo katika maeneo ya kazi na hii nadhani tuliyokuwepo mawizarani tunashuhudia, Mfuko kila baada ya kipindi wanapita na kutoa taaluma kwa wafanyakazi. Lakini vile vile wanapita pia katika Mashirika na katika taasisi za sekta binafsi. Lakini pia mafunzo au taaluma inatolewa kupitia vipindi vya redio na vipindi hivi vinatoka kila wiki mara moja, pia vinatolewa kwa njia ya televisheni, vipeperushi, pia kupitia maonesho na makongamano mbali mbali ambayo *ZSSF* inakuwa inashiriki.

Nichukue tu kwamba jambo la taaluma ni jambo jema, na Mfuko utazidi kutoa taaluma hiyo hasa katika marekebisho haya ya sheria yaliyofanyika. Kazi hiyo tutaendelea kuifanya na itafanyika kwa juhudi zaidi, kwanza kujenga uelewa wa marekebisho yenyewe ya Sheria, lakini vile vile kufahamu kwa undani faida zitakazopatikana kwa wananchi kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

La pili ambalo hili lilizungumzwa na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) alitaka kwamba Mfuko utizame uwezekano wa kuwekeza katika kuendeleza viwanda nchini. Hapa niseme tu Mfuko hivi sasa unashirikiana kwa karibu zaidi na Mifuko mengine iliyokuwepo Tanzania Bara hasa kupitia umoja wao ambao unaitwa Umoja wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*TSSA*) kwa maana ya *Tanzania Social Security Association*. Utafiti huo unafanyika kwa Tanzania Bara na Zanzibar na kubwa unalenga katika kuangalia maeneo ambayo mifuko iweza kuwekeza katika kuendeleza sekta ya watu wake.

Kwa hiyo yapo maeneo mengi yanaangaliwa likiwemo eneo la uvuvi hasa uvuvi wa bahari kuu, kusindika mazao ya samaki, mwani na mazao mengine kama alivyotaja Mheshimiwa Mwakilishi.

Mhe. Naibu Spika, matokeo ya utafiti huo ndiyo yatakayoiongoza Mifuko hii kuona ni maeneo gani ya kuwekezwa katika kuendeleza viwanda hapa nchini na hiyo itatoa fursa ya kukuza uchumi, lakini vile vile itatoa fursa za ajira hasa kwa vijana, ambao Sekta ya Maendeleo ya Viwanda inatarajiwa kuwa ndiyo sekta itakayosaidia zaidi kuchangia katika kuondosha tatizo la ajira kwa vijana wetu hapa. Suala hilo linashughulikiwa lakini hata hapa kwetu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetoa fursa hiyo kwa Mfuko wetu wa *ZSSF*, kuangalia uwezekano wa kuwekeza hasa kwenye eneo la uvuvi wa bahari Kuu. Kwa hivyo hili linafanyiwa kazi na naomba Mheshimiwa aelewe tu kwamba mifuko hii iko kwa ajili ya maendeleo ya nchi na maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Rashid Shamsi, yeye alitaka niwatoe hofu wafanyakazi kwamba mabadiliko haya ya Sheria hayatokuwa na madhara kwao. Vile vile niunganishe na suala la Mhe. Machano Othman Said yeye alitaka ufafanuzi zaidi wa kujua ni kwa kiasi gani mfanyakazi ataweza kuathirika au ni mapato gani mfanyakazi kabla ya marekebisho angeweza kuyapata, ambao mafao yake na yale ambayo anaweza kuyapata baada ya Marekebisho ya Sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, tukichukulia mfano kwamba mfanyakazi anapata mshahara wa shilingi laki tatu (300,000) na anachangia kwa muda wa miaka 15, sasa la mwanzo linafanyika ni kutafuta ile pencheni kamili na hii inapatikana kwa kuchukua mshahara wake unazidisha mara miaka aliyochangia (15), unazidisha mara 12 na unagawa kwa 30, utakapopata jumla yake utapata pencheni kamili ambayo mfanyakazi anastahiki kwa mwaka. Sasa hii pencheni ambayo mfanyakazi anastahiki kwa mwaka tunachukua *two third* ndizo tutakazo zi-*convert* kwamba ni pencheni yake ya kila mwezi na ile *one third* ndiyo itakayokuwa kiinua mgongo chake.

Lakini kwenye hii pencheni ya mwezi tukichukua *two third* tunaigawa kwa 12, kwa hivyo unapata pencheni ya kila mwezi na ile *one third* tunazidisha na *factor* ya 20 kupata mafao yake kwa maana ya kiinua mgongo. Sasa kwa mtu ambaye anapata laki tatu (300,000) hivi sasa kwa *formula* iliyopo kabla ya marekebisho atakuwa anapata pencheni ya mwezi ya laki moja (100,000), lakini kiinua chake mgongo kitakuwa ni milioni 12 na jumla ya michango yake yote ni shilingi milioni nane na laki moja (8,100,000), kwa hivyo kwa muda wake wote wa miaka 15 huyu mtu atakuwa kachangia milioni nane na laki moja (8,100,000) lakini mafao yake ya kiinua mgongo atapata milioni 12, na kila mwezi atakuwa anapata pencheni ya shilingi laki moja (100,000).

Mhe. Naibu Spika, kwa *formula* mpya ambayo *formula* hii kwa mshahara ule ule, na kwa miaka ile ile 15 pencheni yake kwa mwezi itakuwa ni laki moja na ishirini elfu, (120,000), imetoka kutoka laki moja mpaka laki moja ishirini elfu (120,000) kiinua chake mgongo kitashuka kitakuwa ni milioni saba na laki mbili (7,200,000). Lakini ukichukua *formula* ya kwamba huyu mtu tunamtarajia ataishi baada ya kustaafu, hizi ni *calculations* anaweza akaishi kwa siku moja zaidi ya hicho kipindi ambacho sisi tunampangia, sisi hatuna *control* hiyo ya maisha ya mtu, ni wastani unaochukuliwa katika Mifuko yote, ni kwamba huyu mtu ataweza kuishi baada ya kustaafu miaka 60 anaweza kuishi kwa miaka 20 zaidi, wengine wanafika 12, wengine 10, wengine 20, wanapishana.

Sasa ukichukua jumla atakayopata kwa *formula* ya zamani atakuwa huyu mtu anapata milioni 12, lakini ukichukua kwa *formula* hii mpya, ukijumlisha ile pencheni ya kila mwezi kwa muda wa miaka 20 mbele, ukijumlisha na kiinua mgongo chake atakuwa ana wastani wa milioni kumi na moja na laki mbili (Sh 11,200,000) kwa hivyo mapishano siyo makubwa, jumla ya yale mafao, atapoteza kama laki nane (800,000) kimahesabu. Lakini kuna faida ya hii na faida ambayo ataipata huyu mtu ni kwamba ukimpa pesa zake zote kwa wakati mmoja kuna uwezekano wa kuzitumia fedha zake zile zote na maisha yake katika kipindi chote cha kustaafu akawa katika hali ngumu ya kimaisha. Lakini unazichukua kutoka kwenye kiinua mgongo unazipeleka kwenye pencheni ya kila mwezi. Kwa hivyo kwa mfanyakazi tutakuwa tumemsaidia sana kwenye hili, kwa sababu atakuwa anapata kila mwezi pencheni yake ya laki moja ishirini elfu badala ya laki moja ambayo anaipata sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, hesabu hizi naomba ziwaeleweshe Waheshimiwa Wajumbe waondokane na wasi wasi, lakini vile vile mfuko kama nilivyosema mwanzo utapita kutoa taaluma na kuwafahamisha wafanyakazi kwamba hawatopoteza kiasi kikubwa hicho isipokuwa watakuwa na faida, kwa sababu pencheni zao zitaongezeka ingawaje kiinua mgongo kitapungua, na kupungua kwa kiinua mgongo ni zile pesa tumezitoa huku tumezi - *spread* kwenye kile kipindi ambacho atakuwa kwenye pencheni.

Mhe. Naibu Spika, kuna swali liliulizwa na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kupitia swali lake alilolileta kwa maandishi la kwamba wanawake hasa katika sekta ya elimu alisema wanazeeka haraka sana kutokana na majukumu yao waliyonayo.

Nimuhakikishie kutokana na tafiti mbali mbali zilizofanyika inajulikana dunia nzima kwamba wanawake wanaishi zaidi kuliko wanaume na wastani wa maisha sasa hivi *life expectancy* imepanda na imefikia karibu miaka 72. Lakini wanawake kuna *study* zilizofanyika baada ya kustaafu kwa lazima miaka 60 wana uwezo wa kuongeza miaka 20 zaidi na wakafika 60 na 20 ikawa 80 kuna uwezekano huo, lakini kwa wanaume wanaongeza labda kwa miaka 18 kwa wastani, kwa hivyo miaka miwili tafauti, wanawake wanaishi zaidi kuliko wanaume, kwa hivyo tusiwe na wasi wasi na hilo.

Pia ipo fursa kwa wanawake wanaotaka kustaafu mapema wanaweza kustaafu katika umri wa miaka 55 sawa sawa na wanaume na hii imewekwa baada ya wanawake kulalamika wakati huo walikuwa wakistaafu katika umri wa miaka 50, sasa tumeweka pamoja na kwa kutizama life *expectancy* wanawake

wanaishi zaidi, kwa hivyo ni busara pia tukawa na muda sawa wa kustaafu kwa jinsia zote. Kwa hivyo hili Mhe. Riziki usiwe na wasi wasi nalo.

Mhe. Shamsi alitaka kujua wale watakaostaafu kabla ya kupitishwa rasmi kwa sheria hii. Niseme kwamba sheria hii itaweka mpaka wale ambao sheria haijapitishwa hawatahusika na mabadiliko haya, watakaohusika ni wale ambao mara tu baada ya sheria hii itakapowekwa saini na Mhe. Rais na kuwa sheria kamili inatumika, hao sasa kuanzia hapo watakaostaafu hapo wataguswa na sheria hii, wale wengine wote wataendelea na utaratibu ule ule kama sheria ya zamani ilivyo.

Pia Mhe. Shamsi, ulizungumzia suala la kifungu cha 26(3) cha Waziri kuahirisha mafao kwa kushauriana na Bodi, lakini pia na Mhe. Machano Said alikuwa na hoja ya kusema bodi inamshauri Waziri au Waziri ashauriane na Bodi. Suala si nani anamshauri nani, suala ni uwezo, na uwezo wa kufanya mabadiliko upo kisheria ndani ya sheria hii kwa Waziri kupitia kutunga kanuni zake. Sasa hilo lisiwe na wasi wasi, ikiwa Waziri anashauriwa, ikiwa Waziri anashauriana haina tatizo, lakini mwisho wa habari ni kwamba Waziri ndio mwenye uwezo kwa mujibu wa sheria na kwa kupitia kanuni atakazozitunga kuweka mabadiliko au utaratibu wowote utakaoonekana unastahiki.

Lakini hili la kuahirisha mafao tulisema kwamba liwekewe muda maalumu. Hapa naomba Mhe. Naibu Spika, nieleze kwamba, sheria ya sasa imeweka utaratibu huu wa kutoweka muda kwa mazingatio maalumu na mazingatio yenyewe ni kwamba. Kwa mfano sheria ya sasa iliweka mafao matano nayo ni :-

- Mafao ya Uzeeni
- Mafao ya Ulemavu
- Mafao ya Matibabu
- Mafao ya Uzazi

Ilivyoanza kutumika sheria hii mafao ya matibabu na uzazi yaliahirishwa kwa sababu ya kuweka mazingira, kwanza kuyajua mazingira yenyewe yalivyo kabla hujautumbukiza mfuko huu kwenye shughuli ambayo italeta hasara na mfuko kuathirika. Kipengele hichi kimeweka makusudi Waziri ashauriane na halazimiki kushauriana na Bodi na kushauriana na watu wengine wowote hata wadau wengine, lakini tutakapoamua kuingiza fao, basi lile fao kwanza liweze kuwa endelevu lakini lisije likawa na athari kwenye mfuko wenyewe. Kwa hivyo hiyo imewekwa maalumu na kwa sasa hivi ndio kabisa tusiwe na wasi wasi, kwa sababu takriban katika mafao matano yaliyokuwemo kwenye sheria mafao manne yote *ZSSF* sasa hivi wanayatoa. Wanatoa fao la Uzeeni, wanatoa

fao la Urithi la Ulemavu na tayari fao la Uzazi linatolewa, lililobaki sasa hivi ni fao la Matibabu na hili ni kutokana na ugumu wake. Vile vile na hata washauri wengi waliokuja kufanya tafiti nyingi zilizofanyika kwenye mfuko huu, walishauri kwamba suala hili tuliingie kwa tahadhari kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa serikali imeunda Kamati ambayo inashughulikia suala hili la kuhakikisha kwamba tunaingia katika masuala ya Bima ya Afya, inazingatiwa na Kamati hiyo na mara baada ya Serikali kupata ripoti ya Kamati suala hili litazingatiwa na kuona kama *ZSSF* itaweza kuingia au kuliingiza fao hili la matibabu. Lakini kama tahadhari tu mifuko ya wenzetu Tanzania Bara hivi sasa wanalitoa fao la matibabu kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, wanalitoa na kulihamishia kwenye Bima za Afya kwa mfano *NHIF*, hawajazitoa mpaka sasa hivi lakini wamo katika taratibu na *process* ya kuhamisha fao hili kulipeleka huko. Sisi tunasubiri matokeo ya *study* inayofanywa na matokeo yatatushauri nini la kufanya wakati *study* hiyo itakapokamilika.

Kuna suala jengine liliulizwa la mikopo na hili liliulizwa na waheshimiwa wengi; Mhe. Riziki, Mhe. Machano Othman Said, ninafikiri hata Mhe. Shamsi alilizungumza suala la mikopo, kwamba kwa nini Taasisi za Serikali na Serikali zinakopa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na iwapo kwamba Mfuko pia unakopesha watu binafsi.

Kwanza niseme Mfuko haujawahi kukopesha mtu binafsi hata mara moja, kwa hivyo hakuna mtu binafsi aliyewahi kukopeshwa au kukopa kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Lakini suala la Serikali na Taasisi zake kukopa hili ni suala la kawaida, katika mifuko yote duniani na kwa sababu moja ya jukumu la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni kuziwekeza fedha zake na kuziwekeza katika *real estate* katika masoko ya fedha lakini pia katika utoaji wa mikopo.

Hapa niseme kwamba katika mikopo yote inayotolewa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii mikopo ambayo inatolewa kwa riba kubwa ni mikopo inayokwenda kwenye Taasisi za Serikali. Serikali inapokopa inakopa kwa asilimia 18 hivi sasa, lakini ukiwekeza fedha hizi kwenye *fixed deposit*, *return* inayoipata ni asilimia 9 mpaka 12. Kwa hivyo bado mkopaji Serikali analipa zaidi kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kwa hivyo naamini kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ingependa zaidi Serikali ikope, kwanza kuna usalama. Katika nchi nyengine Serikali inakopa mpaka kufikia asilimia 70 ya mikopo inayotolewa na Hifadhi ya Jamii. Kwa hivyo hilo si tatizo kwa Serikali kukopa, na mimi naamini kabisa kama Serikali inahitaji kukopa basi wenzetu hawa waisikilize

vizuri zaidi, kwa sababu mikopo yao iko salama lakini pia wanapata faida kubwa zaidi.

Mhe. Machano Othman Said kuna mambo mengi alishauri lakini moja alishauri kuhusiana na kufuatiliwa wale waajiri wasiofuata sheria. Utaratibu upo na *ZSSF* inashirikiana na Idara ya Kazi, inashirikiana na Ofisi ya *DPP*, inashirikiana na Jeshi la Polisi, *TRA*, *ZRB* na *ZIPA*, na huwa wana vikao vya pamoja katika kuhakikisha kwamba wanafuatilia kwa wale waajiri ikiwa katika Sekta ya Uwekezaji na kuona kwamba wana-*comply* na sheria zote zilizopo nchini ikiwemo Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Hivi sasa tuna utaratibu ambao unaandaliwa wa kupata taarifa za waajiri wote kupitia vitambulisho vya Mtanzania, kupitia *NIDA* lakini vile vile na *ZAN ID*. Hii itatusaidia kuwatambua waajiri wote walioko katika sekta binafsi na wale waajiriwa walioko katika Serikali.

Pia kulikuwa na suala la taarifa za mwenendo na mchanganuo wa michango ya waajiriwa au wachangiaji. Hili pia liliulizwa na Mhe. Machano Othman Said lakini pia Mhe. Mohammed Ahmada aliligusia suala hili na kutaka kwamba wanachama ama wachangiaji wawe wanapewa taarifa kila mwezi.

Hivi sasa upo utaratibu ambao mtu anapotaka kupata taarifa ya mwenendo wa uchangiaji wake akienda *ZSSF* anapewa taarifa hiyo. Lakini pia taarifa hizi sasa ziko kwenye *website*, kwa hivyo wafanyakazi wanaweza ku-*access* taarifa zao kwenye *website* ya *ZSSF* ambayo ni www.zssf.org, lakini kwa kusaidia wale wenzetu ambao wanaishi katika maeneo ambayo si rahisi kupata mitandao hii basi pia *ZSSF* inakusudia kuandaa utaratibu wa kupeleka taarifa hizo kupitia *SMS*. Kwa hivyo mtu akiwa na simu yake anaweza ku-*access* taarifa yake ya jinsi anavyochangia katika mfuko.

Kuhusu mikopo kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Mhe. Naibu Spika, na wanafunzi, kwamba kuna ushauri ulitoka hapa na Mhe. Machano aliutoa ushauri huo lakini pia na Mhe. Riziki aligusia kwenye suala la mikopo kwa wanafunzi na wakataka kwamba mfuko uandae utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi lakini pia kwa waheshimiwa.

Ni jambo zuri lakini tuseme tu jukumu la msingi la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii sio kutoa mikopo. Jukumu la msingi la mifuko hii ni kukusanya michango kuiwekeza michango hii na baadaye kutoa mafao yanayostahiki kwa wachangiaji wake. Lakini *ZSSF* iko tayari kushirikiana na Taasisi yoyote ya kifedha kwa makubaliano maalumu, lakini shughuli ya utoaji wa mikopo basi

itolewe na taasisi hiyo ya kifedha, kwa sababu kwanza ndio shughuli yake lakini pia ina ujuzi na uzoefu wa kuendesha mikopo sio *ZSSF*.

Kwa hivyo kama iko benki au taasisi nyengine yoyote ya fedha ambayo inataka kushirikiana na *ZSSF* tunawakaribisha waje kufanya mazungumzo na *ZSSF*, na naamini watafikia makubaliano basi utaratibu wa mikopo hiyo iwe kwa waheshimiwa au iwe mikopo kwa wanafunzi inaweza kutolewa. Hivi sasa mfuko tayari uko kwenye makubaliano na Benki ya Posta ya Tanzania (*Tanzania Postal Bank),* na inaendesha utoaji wa mikopo kwa wastaafu. Kwa hivyo hawa *pension* yao wameji-*organize* kupitia benki hii, *ZSSF* inatoa fedha hizo lakini mikopo hiyo inakuwa *administered* na *Tanzania Postal Bank*. Kwa hivyo fursa hiyo ipo, tunawaomba tu benki ambayo itakuwa tayari basi wafanye mazungumzo na *PBZ* katika suala hilo.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi alizungumzia suala la mikopo ya nyumba na nimjulishe tu Mhe. Dkt. Makame kwamba kifungu 41(2) kimetoa pendekezo hilo wazi wazi kwenye haya marekebisho ya sheria, kwamba Waziri kwa kushauriana na Bodi, kupitia kanuni, anaweza kuweka utaratibu maalumu kwa wanachama kutumia stahiki zao kama dhamana ya kupata mikopo (*guarantee)*. Kwa hivyo fursa hiyo ipo na anaweza kukopa ile stahiki yake kwa asilimia isiyozidi 50. Kwa hivyo fursa hii ipo kama anataka kukopa pindi ikipita sheria hii ya stahiki yake yaani hakopeshwi na *ZSSF*, *ZSSF* inatumia ile fedha yake, ile stahiki yake kama dhamana kwa kumuwezesha yeye kupata mikopo kwenye taasisi zinazotoa mikopo. Suala hili pia liliulizwa na Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, ninaamini na yeye itakuwa tayari nimeshampatia ufafanuzi wa suala hili.

Mhe. Maudline Cyrus Castico alizungumzia suala la *house girls* kama na wao wanaweza kupata fursa hii, fursa hii ipo kwa kila mtu. *House girls* wako kwenye sekta isiyo rasmi, na Sekta isiyo Rasmi kwa mabadiliko ya sheria hii yanaingiza makundi hayo. Wafanyakazi walio kwenye Sekta Binafsi, wafanyakazi walioko kwenye sekta ya umma lakini na wafanyakazi walioko kwenye Sekta isiyo rasmi wote wamo na wale wanaoishi nje ya nchi, *diaspora*, wote wamo humo na wastaafu kama sisi sote tunaingizwa chini ya marekebisho ya sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo na ninaamini kwamba nimegusa yale yote muhimu yaliyoguswa na waheshimiwa wajumbe, lakini pia nasema kama yale yote yaliyotolewa kama michango ya kutusaidia katika uendeshaji wa mfuko huu baada ya kupitishwa sheria nayo tunayachukua.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2016

Sehemu ya Kwanza

Kifungu 1	Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2	Kusomwa

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Sehemu ya Pili

Vifungu vya Marekebisho

Kifungu 3	Marekebisho ya Kifungu cha 2 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 4	Marekebisho ya Kifungu cha 12 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 5	Marekebisho ya Kifungu cha 17 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 6	Marekebisho ya Kifungu cha 23 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 7	Marekebisho ya Kifungu cha 26 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 8	Marekebisho ya Kifungu cha 29 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 9	Marekebisho ya Kifungu cha 31 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 10	Marekebisho ya Kifungu cha 32.
Kifungu 11	Marekebisho ya Kifungu cha 41 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 12	Marekebisho ya Kifungu cha 42 pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 13	Marekebisho ya Kifungu cha 44 pamoja na marekebisho yake.

Jadueli la kwanza pamoja na marekebisho yake.

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

\

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2016

(Kusomwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2016 usomwe kwa mara ya tatu.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Kwa kuwa shughuli zetu za leo zimefikia mwisho sasa ninafikiri kwanza nisome tangazo ambalo limetoka kwa Kaimu Katibu wa Baraza ambalo linasema kwamba ninawatangazia wajumbe wote wenye nia ya kugombea nafasi mbali mbali katika Umoja wa Wabunge Wanawake wa Nchi za Jumuiya ya Madola *CWP* na Umoja wa Mabunge ya Nchi za Jumuiya za Madola *CPA* Tawi la Zanzibar kuwa fomu zinapatikana katika Ofisi ya Katibu wa Baraza kuanzia leo na mwisho wa kurejesha fomu hizo ni kesho tarehe 29/11/2016 saa 11.30 jioni.

Nafasi zinazogombewa ni kama ifuatavyo:-

Kwa *CPA*; Mwenyekiti, Makamo Mwenyekiti, Wajumbe watatu wa Kamati Tendaji, na Muweka Hazina. Uchaguzi wa nafasi hizi utafanyika Alkhamis tarehe 1/12/2016 mara baada ya marekebisho ya Kanuni.

CWP; Wajumbe ambao watagombea ni Mwenyekiti, Makamo Mwenyekiti, na Wajumbe 3 wa Kamati Tendaji. Uchaguzi wa nafasi hizi utafanyika Jumatano tarehe 30/11/2016 mara baada ya kuahirishwa kwa kikao cha asubuhi. Ahsanteni.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya tangazo hili natangaza kuahirisha kwa kikao hiki hadi kesho asubuhi saa 3.00.

(Saa 11.33 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 29/11/2016 saa 3.00 asubuhi)